epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumatano Aprili 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581642

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**TCB** yatenga bil. 300/- kunufaisha wafanyabiashara na kuongeza ajira

UKURASA 4



**Tuhuma** uhujumu wa mali za AICC zang'oa vigogo

UKURASA 9



**Bei** ya petroli, dizeli yapanda visiwani Zanzibar

UKURASA 17

**RODRYGO AFUNGUKA KUIKATALIA LIVERPOOL**

UKURASA 22

# Hali tete Rufiji

• **Watu** 10,000 wakosa makazi, mifugo na mali vyasombwa na maji...

*Endelea ukurasa 3*



## 30 mbaroni kwa tuhuma za kutaka kupata mafao ya udanganyifu NSSF

UKURASA 5



Kwa kikokotoo cha zamani, mstaafu aliyekuwa na mshahara wa Sh. 800,000, angepata mafao ya Sh. milioni 57, lakini kwa kikokotoo kipya atapata Sh. milioni 28.

**Mrisho Gambo**



Watumishi wanahitaji wapate mafao yao kupitia kikokotoo cha asilimia 50 na si hiki cha asilimia 33. Maumivu ni makubwa.

**Dorothy Semu**



Tulikuwa na kikokotoo cha asilimia 24, tukaja cha asilimia 50 hadi hiki cha sasa cha asilimia 33 ambacho kimeonekana kuwa tatizo kubwa kwa wastaafu.

**Tumaini Nyamhokwa**

## TUCTA yaliachia Bunge hatima kikokotoo mafao

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA: NI USHINDI TU LEO KOMBE FA UK.24

**KATUNI** UK.6



Msafara wa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Mboni Mhita ukipita moja ya barabara iliyofurika maji wakati akitokea kata ya Lunguya, Halmashauri ya Msalala kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wawekezaji wazawa wa kiwanda cha kuchakata madini ya dhahabu, juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Mshtakiwa aeleza alivyomwingiza mpenziwe biashara dawa kulevya

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Salim Jongo anayetuhumiwa kusafirisha dawa za kulevya aina Heroin kilo 51.47 na wenzake watatu, ameeleza alivyomwingiza mpenzi wake kwenye biashara ya dawa za kulevya bila mwenyewe kujua hadi kukamatwa na askari.

Ameeleza kuwa mpenzi wake huyo, Tatu Nassoro ambaye ni mshtakiwa wa nne katika kesi hiyo, alikuwa hajui chochote kuhusu biashara hiyo na Salim alikuwa anaficha dawa hizo na fedha kwenye upande mmoja wa kabati la nguo, kabati hilo lilikuwa na milango mitatu.

Hayo yalielezwa jana na Mawakili wa Serikali, Cathibet Mbilingi na Groly Kimaro mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ajali Milanzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakati washtakiwa Salim, Ernest Semagoya, Amini Sekibo na Tatu wakisomewa maelezo ya mashahidi baada ya upelelezi wa kesi hiyo kukamilika.

Mawakili hao walidai kuwa maelezo hayo yalitolewa na mshtakiwa wakati akihojiwa na askari polisi baada ya kukamatwa na kukiri anahusika na biashara hiyo aliyoshawishiwa kuingia na rafiki yake Semagoya katika kesi hiyo aliyemtaka kuwa msiri kwa kutokumwambia mtu yeyote na pia atafute sehemu ya kuficha mzigo wake.

"Septemba 7, 2020 nilichukuliwa na kupelekwa Kituo cha Polisi Tazara, Septemba 8, 2020 tulichukuliwa mimi pamoja na Sekibo kwenda nyumbani kwa mpenzi wangu Tatu, niligonga mlango akafungua, tukaingia ndani tukiwa na askari polisi.

"Huu mzigo ambao nilikuwa ninauhifadhi hapa kwako bila wewe kujua zilikuwa ni dawa za kulevya, kwahiyo tupo chini ya ulinzi pamoja na Sekibo," alidai Salim katika maelezo yake.

Alidai kuwa hakuwahi kumweleza mpenzi wake Tatu kuhusiana na biashara hiyo hadi siku ambayo alikamatwa. Askari walikuta kilo hizo za Heroin pamoja na Sh. milioni 58 ambazo hakujua kama zilikuwa ndani kwake kwenye kabati.

Inadaiwa Septemba 18, 2020, eneo la Temeke Vetenari washtakiwa hao walikutwa wakiendesha biashara haramu ya dawa kulevya aina ya Heroin kilo 51.47 kinyume cha sheria.

# TUCTA yaliachia bunge hatima kikokotoo

**Na Vitus Audax,** DODOMA

WAKATI Bunge likiendelea kupokea michango na hoja mbalimbali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Bunge kwa mwaka 2024/25, kikiwamo kikokotoo cha mafao ya wastaafu, Shirikisho la wafanyakazi Tanzania (TUCTA) limeliacha suala hilo mikononi mwa Bunge.

Aidha, wabunge wameendelea kusisitiza kuwa ni vyema serikali ikarejea mezani kuzungumza na vyama vya wafanyazi ikiwamo kuzifumua kanuni za ukokotoaji mafao na wengine wakisema irejeshe kikotoo cha mwaka 2017 cha asilimia 50.

Akizungumza na mwandishi wa Habari hii jana, Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, alisema suala la kikokotoo halijawahi kuwa rafiki kwa mtumishi yeyote kutokana na kugusa moja kwa moja maslahi kwa kupunguza mafao yao na haliwezi kukubalika hata siku moja.

"Hadi kufikia hapo suala hilo tumekuwa tukilipigania kwa miaka mingi tangu kile kikokotoo kilichokuwa kikichukua asilimia 24, tukaja cha asilimia 50 hadi hiki cha sasa cha asilimia 33 ambacho kimeonekana kuwa tatizo kubwa kwa wastaafu," alisema Nyamhokya.

Alisema kwa sasa kama viongozi wa shirikisho hawana mchango zaidi kwa suala hilo, hivyo wanaliachia Bunge kumalizana nalo huku wao (TUCTA) wakiendelea na majadiliano na uongozi na ifikapo Mei Mosi, mwaka huu, watatoa tamko rasmi.

"Tunajua kuwa hii ni mifuko yetu na ni kwa ajili ya manufaa ya watumishi wote lakini wanaotunza fedha ni serikali. Tunaendelea kukaa nao kujadiliana na kukubaliana ni lipi linaweza kufanyika bila kumwumiza mfanyakazi," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU) Dk. Paul Loisulie, alisema mjadala kuhusu Kikokotoo umekuwapo kwa muda mrefu tangu mwaka 2005.

Alisema msingi wa mjadala wa sasa ni baada ya kuunganishwa mifuko mwaka 2018 na baadaye kusawazishwa kikokotoo hatua ambayo imeshusha viwango vya malipo ya mkupuo na ya kila mwezi.

Alitaja sababu za kuunganishwa mifuko na kuleta kikokotoo kipya ni mifuko ya Watumishi wa Umma (PSPF), Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (LAPF), Wafanyakazi wa mashirika ya Umma (PPF) na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambayo ilidaiwa kuwa ilikuwa hoi kutokana na madeni makubwa inayodaiwa serikalini, uwekezaji usio na tija, matumizi mabaya ya fedha na mwingiliano wa uamuzi wa kisiasa.

"Uamuzi uliofanyika ili kunusuru mifuko umeleta maumivu makubwa kwa watumishi wanaostaafu na kwa sasa unahitajika mjadala mpana wa wazi utakaojumuisha wadau wote ili kufikia uamuzi wenye tija," alisema.

Pia alisema inatakiwa kuimarisha usimamizi wa mifuko ili kuondoa matumizi mabaya ya pesa pamoja na uwekezaji usio na tija.

**UPINZANI WANENA**

Viongozi wa vyama vya upinzani nao wameibuka na kusema endapo kikokotoo cha sasa kitaendelea kama kilivyo, muda si mrefu kitakosa mvuto na kutokuaminiwa tena na watumishi.

Kiongozi wa ACT Wazalendo, Dorothy Semu, alisema mara kadhaa chama hicho kimekuwa kikiishauri serikali kukaa upya na kurejesha kikokotoo kilichokuwa kikitumika mwaka 2017 cha asilimia 50 ili kuondoa maumivu wanayokabiliana nayo wastaafu kwa sasa.

"Watumishi wanahitaji wapate mafao yao kupitia kikokotoo cha asilimia 50 na wala si hiki cha asilimia 33. Maumivu bado ni makubwa tuna wasiwasi kwamba mifuko hii itapoteza uaminifu tena kwao watakapokuja na hoja kuwa pensheni haipo bali ni maumivu," alisema Semu.

Waziri Mkuu Kivuli wa chama hicho, Isihaka Mchinjita, alisema baraza hilo la mawaziri kivuli, linamshauri Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kupeleka bungeni mabadiliko ya kanuni hiyo ya mwaka 2023 na kurejesha kanuni ya mwaka 2017 ambayo inakubalika kwa watumishi wote.

Alisema baraza hilo linaendelea kuishauri serikali kuendelea kuajiri na kuwa na watumishi wakutosha ili kuongeza idadi ya wachangiaji katika mifuko hiyo kwani kwa sasa waajiriwa ni wachache na idadi ya wastaafu inaendelea kuongezeka hali inayopunguza namba ya wachangiaji.

"Pia tunapendekeza mifuko hii iache kutegemea moja kwa moja fedha kutoka kwa wachangiaji bali ikae na kuona namna ya kuwekeza katika mifumo na bondi ili mifuko ipate faida na kuanza kulipa kutokana na matokeo ya uwekezaji tofauti na sasa inavyolipa kutokana na fedha za wachangiaji," alisema.

Mchinjita alisema kikokotoo kipya si mpango wa watumishi bali ni wa serikali baada ya serikali kukopa fedha bila kuirejesha katika mifuko hiyo, hivyo ni vyema serikali irejeshe fedha hizo ili kuondoa maumivu kwa wastaafu.

**KAULI YA GAMBO**

Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, wakati akichangia makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu, alisema wastaafu mbalimbali wanaendelea kulia na kikokotoo kutokana na kikokotoo cha sasa.

"Nimepitia kanuni mbalimbali kama vile hii ya Mei 2022 ya Agosti 12, 2018, kanuni ya SCRA 2017 na 2018 pia na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge 2017 pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani ya 2017.

"Kikokotoo kilichokuwapo hadi mwaka 2014 kilikuwa kizuri na ndicho Watanzania wengi wanakitaka. Chenyewe kilikuwa kimechukua asilimia 50 na kilionyesha miaka ya kuishi baada ya kustaafu kuwa ni 15 na nusu. Pia kilichukua mshahara wa mwisho wa mfanyakazi ambao mara nyingi huwa ni mkubwa," alisema Gambo.

Pia alisema kwa sasa kikokotoo kimepungua kutoka 1/540 hadi 1/580 pia wamechukua wastani wa miaka 10, wakitafuta miaka mitatu iliyo bora ambapo kwa kawaida lazima mshahara utapungua na kuathiri mafao. Pia miaka ya kuishi imepunguzwa hadi 12, kitu alichodai si sahihi.

"Nimechukua mfano, sampuli ya mishahara na nimefanya mahesabu kwa mtumishi ambaye anastaafu akiwa na mshahara Sh. 800,000. Kwa kikokotoo cha kabla ya Julai 2014 katika mfuko wa LAPF na PSPF, alikuwa anapata Sh. 57,466,666 na kwa kikokotoo cha sasa anapata Sh. 28,675,862 tofauti ya Sh. 29,190,804. Kwa mwezi atapata Sh. 401,000 kwa kikokotoo cha zamani na cha sasa atapata 388,137," alisema Gambo.

Alisema katika hali ya kawaida kwenye kikokotoo hicho yamefanyika makosa makubwa kwa kuwa sheria inayoanzishwa inatakiwa kuanzia pale tu ilipotungwa. Kwa hiyo, wote ambao sheria hiyo iliwakuta walitakiwa kulipwa kwa kikokotoo cha zamani na kipya kusubiri wale watakaoanza kazi.

HABARI KITAIFA

# Hali tete wilayani Rufiji, mafuriko yakiacha watu 10,000 bila makazi

**Na Halfani Chusi**

ZAIDI ya kaya 2,500 katika Kata ya Muhoro, wilayani Rufiji, mkoani Pwani zimeathiriwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini.

Imeelezwa kuwa mafuriko hayo yamesababisha zaidi ya wananchi 10,000 kukosa mahali pa kuishi.

Diwani wa Muhoro, Abdul Chobo, akizungumza na Nipashe kwa simu jana, alisema mafuriko hayo yamewaacha katika hali ngumu kwa kuwa wengi wao hawana mahali pa kushi, huku mali na mashamba yao yakiharibiwa na maji.

Alisema kata yake ina vijiji sita na vitongoji 27. Kati ya vitongoji, viwili ndivyo havijakumbwa na maafa, lakini vilivyosalia vimeathiriwa.

Alisema wananchi waliokosa makazi kutokana na mafuriko ni wengi, wakihifadhiwa shuleni na wengine kupata hifadhi kwa ndugu.

"Kuna baadhi ya shule za msingi zimezingirwa na maji. Kwa mfano, Shule ya Msingi Muhoro imefungwa na nyingine wataalamu wanaendelea kufanya tathmini kuona kama zitafungwa au la.

"Kuna watoto wa sekondari wanaohitaji kuvuka maji ili wafike shuleni na kurudi majumbani, lakini wameshindwa kutokana na mafuriko. Wananchi wengi wamepoteza mazao, mashamba na mifugo yao," alisema diwani huyo.

Chobo alisema kuwa awali Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) ilitahadharisha na kuwataka kuchukua hatua za kuhama, lakini wengine walipuuza ingawa kuna wachache waliochukua hatua na wameepuka madhara hayo.

Alisema kutokana na mvua ilivyokuwa inanyesha kwa wingi, walitarajia kupata mafuriko hayo tangu Desemba mwaka jana, lakini kuwapo Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), kumesaidia kuzuia athari zaidi.

Hata hivyo, kuna dhana kwamba kufunguliwa kwa milango ya bwawa hilo kumesababisha hali inayoshuhudiwa sasa Rufiji.

"Hatuwezi kusema bwawa limesababisha mafuriko, si mara ya kwanza kutokea. Mara ya mwisho yalitokea mwaka 2020. Je, kulikuwa na bwawa? Je, na yale yaliyotokea mwaka 1978 na 1998 yalisababishwa na bwawa? Kwahiyo, bwawa si sehemu ni matokeo ya mvua kubwa na asili ya Rufiji," alisema.

Diwani huyo alisema kilio kikubwa kwa sasa ni chakula na makazi mengine ya dharura, ili waliothiriwa wapate mahali pa kujisitiri huku wakisubiri hatua za serikali.

Pia aliomba huduma za afya zisogezwe haraka walioko wananchi hao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko, akifafanua kwamba kutokana na mafuriko hayo, vyoo vingi vimezibuka na hivyo wanakijiji wengi wapo katika hatari ya kupata magonjwa ya mlipuko.

Alipoulizwa kuhusu hatua zilizochukuliwa na serikali mpaka sasa, diwani huyo alisema kuwa kwa mujibu wa mkuu wa wilaya, ofisi ya waziri mkuu imetoa mahindi tani 20 na wahisani mbalimbali wameanza kuchangia misaada ya chakula.

"Serikali, viongozi wa chama, wilaya na mkoa wamefika, timu za wataalamu wa takwimu na sasa mkuu wa wilaya anaendesha kikao kuona kinachopatikana kinawafikia walengwa," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji Cha Muhoro Magharibi ambacho kimeathiriwa na mafuriko hayo, Amina Mnyimwa aliomba serikali ipeleke msaada wa chakula haraka.

Alisema tani zinazohitajika ni nyingi kwa kuwa walioathirika na mafuriko katika kata hiyo ni zaidi ya 16,000.

"Watu wakipata chakula watatulia, kilio kingine ni mazao yao mengi yamepotea, watu wangekuwa wanakula ndizi, mpunga ungekuwa tayari umekomaa, mahindi, ufuta hali ni mbaya sana," alilalama mwenyekiti huyo.

Jana Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilitoa taarifa kwa umma, likisema: "Bwawa la JNHPP limesaidia kupunguza athari za mafuriko. Sababu kubwa ya mafuriko kwenye wilaya za Kibiti na Rufiji ni kuongezeka mtiririko wa maji katika Mto Rufiji kulikosababishwa na mvua kubwa za El-Nino zinazoendelea kunyesha katika mikoa ya nyanda za juu kusini."

Mjumbe wa Kamati Kuu Taifa Chama Cha ACT Wazalendo, Husna Sungura alisema ni muhimu serikali ikachukua hatua za haraka kusaidia waathirika wa mafuriko hayo.

"Wanawake na watoto wanateseka sana, kinamama biashara zimekufa, watoto hawaendi shuleni, wananchi tunalipa kodi, sasa hizo kodi zetu matumizi yake ni wapi kama watu wanapata maafa na hawana pa kukimbilia?" Husna alihoji.


Nipashe MWANGA WA JAMII
The Guardian www.ippmedia.com

Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited



Wapendwa Wateja wetu

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia wikiendi ijayo ya tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya **Nipashe Jumamosi, Nipashe Jumapili na The Guardian on Saturday** yatakuwa yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Subscription: 0625 174 714
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

# TCB yatenga bilioni 300/- za kunufaisha wafanyabiashara

**Na Zanura Mollel**

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB), imetenga Sh. bilioni 300 kwa ajili ya mikopo kwa wafanyabiashara wadogo 2,000 nchini, lengo likiwa la kupanua wigo wa ajira na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2024.

Mkakati huo unakwenda kutekelezwa wakati benki hiyo imepata faida ya Sh. bilioni 13.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2024.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Adam Mihayo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utendaji wa taasisi hiyo.

"Tunataka kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya uzalishaji, tumewaona wajasiriamali wadogo watakuwa na faida kwa nchi yetu kwa sababu wanachangia asilimia 30 ya ukuaji wa uchumi," alisema Mihayo.

Alisema kuwasaidia kundi hilo ni kuwajengea uwezo wa mtaji ambako kutawafanya kukua, kuajiri watu wengi zaidi na kupanua wigo wa kodi.

Pamoja na mambo mengine, Mihayo aligusia kuhusu taasisi hiyo kuanzisha huduma ya M-coba, na kueleza kuwa ni jitihada ya benki hiyo kwa kushirikiana na kampuni mojawapo ya mawasiliano ya simu na kufanikiwa kukusanya Sh. billioni 80.

"Hadi sasa tuna wateja milioni 12 ukiachana na hawa waliopo kwenye mfumo wa kidigitali, hata hivyo kwa sasa tunatarajia kufanya uwekezaji mkubwa zaidi kwenye mfumo huo kurahisisha huduma," alisema Mihayo.

Aidha, alisema benki hiyo inatoa mikopo rafiki kwa wastaafu ambao dhamana yao ni pensheni anayolipwa kila mwisho wa mwezi.

Alisema wanachofanya ni kutomsumbua mstaafu kuleta marejesho bali humkata moja kwa moja kupitia michango yao ya kila mwezi wanayoingiziwa kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii.

Katika hatua nyingine, alisema benki hiyo kwa kutambua nafasi ya ajira nchini imetoa ajira kwa mawakala 6,000, ambao wanatarajia kuongeza na kufikia 4,000 kwa lengo la kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma ya benki hiyo.

"Sisi ni namba tatu nchini kwa ukubwa wa matawi, tuna matawi 82, kwa upande wa utoaji elimu na mafunzo tumezingatia hilo kwa wateja wapya na wa zamani kuhakikisha wanapata uelewa wa kukopa na kurejesha," alisema Mihayo.

Kuhusu ukusanyaji wa mapato, alisema umekua kwa kasi kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024 na kufikia Sh. bilioni 56.8 (30%) ikilinganishwa na robo ya kwanza ya mwaka 2023 iliyokuwa Sh. bilioni 43.7.

Alisema TCB inamilikiwa na wanahisa mbalimbali, huku serikali ikiwa na asilimia 83.44, Shirika la Posta (7.61%), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (2.91%), Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) (2.23%), Posta na Simu SACCOS LTD (2.67%) pamoja na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), (1.02%).

Kuhusu maeneo ya kimkakati, alisema wanatarajia kujielekeza kuwafikia wafanyabiashara hususani wadogo, wajasiriamali pamoja na wakulima pamoja na uboreshaji wa huduma za kidijitali.

Kadhalika, alisema mwaka 2025 TCB inatarajia kutimiza miaka 100 tangu ilipoanzishwa mwaka 1925, ikiwa imepitia katika hatua mbalimbali za maboresho.




Meneja Mawasiliano wa Barrick, Georgia Mutagahywa (wa pili kushoto), akikabidhi moja ya vifaa vya kisasa vya kupima ulevi kwa madereva kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Mohamed Bahashwan, vilivyotolewa na kampuni hiyo, kwa Jeshi la Polisi katika Kituo cha Oysterbay, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, SACP, Mtatiro Kitinkwi (kushoto) na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP William Mkonda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Polisi watoa hadhari kwa wazazi, walezi sikukuu ya Eid

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi limetahadharisha wazazi na walezi kuhusu mvua inayoendelea kunyesha kuhakikisha wakati wa kusherehekea sikukuu ya Eid El Fitr, wanalinda watoto wao na kamwe wasishindane na maji.

Wakati tahadhari hiyo ikitolewa, baadhi ya maeneo yakiwamo ya Mkoa wa Pwani, yamekumbwa na mafuriko na kusababisha nyumba kuzingirwa na maji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi hilo, DCP David Misime, wazazi na walezi wanapaswa kuhakikisha wanalinda watoto wao kwa kuwa na mlinzi ambaye ni mtu mzima katika maeneo ambako watoto watakwenda kusherehekea.

DCP Misime alitaka kila mmoja kuzingatia tahadhari zinazoendelea kutolewa kuhusiana na mvua inayoendelea kunyesha.

"Kamwe mtu asijaribu kushindana na maji ya mvua yanayotiririka kwa kasi katika eneo lolote lile kwani kunaweza kuhatarisha maisha," alionya.

Kuhusu sikukuu ya Eid El Fitr na Baraza la Eid, Misime alisema Jeshi la Polisi limeweka mikakati na taratibu za kuhakikisha waumini wa dini ya Kiislamu na Watanzania kwa ujumla wanashiriki ibada na kusherehekea sikukuu hizo katika mazingira ya amani, utulivu na usalama.

Alisema ili mikakati hiyo ilete matokeo hayo, jehsi hilo linatoa wito kwa Watanzania kuzingatia kanuni muhimu ya kiusalama inayosema 'usalama unaanza na mimi kwanza' kwa kujiepusha na vitendo vyote vinavyoleta uvunjifu wa sheria.

Pia alisema kila mmoja anapaswa kuzingatia na kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali zinazosababishwa na uzembe wa kutofuata sheria kama vile mwendokasi.

# DC ashtukia jambo vijana wanaoajiriwa viwandani

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash amesema vijana wa wilaya hiyo wanapaswa kubadilika wanapopata ajira kwa kuacha tabia ya kukimbia kazi baada ya malipo na kurejea pindi fedha zinapoisha.

Okash alitoa kauli hiyo juzi mjini Bagamoyo alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema kwa kufanya hivyo wamekuwa kikwazo kwa wamiliki wa viwanda ambao wanalenga kupata faida katika uzalishaji bidhaa zao viwandani.

"Tuna changamoto ya vijana wetu kwenye sekta ya viwanda wanasubiri muda wakishapewa malipo, huwa wanaondoka pale mshahara. Unapokatika tena ndipo wanarudi kufanya kazi, hii haileti picha nzuri kwa wawekezaji ambao wana malengo yao katika uzalishaji," alisema.

Alifafanua kuwa wawekezaji hao wanajiendesha kwa lengo la wapate faida, hivyo vitendo vya vijana hao vinapunguza uaminifu wa wengine kunufaija na ajira.

"Ukishapewa mshahara huonekani kazini wiki mbili hadi tatu, ni malalamiko makubwa kutoka viwandani na mimi mwenyewe nimeshuhudia, nimeshaita vijana na kuzungumza nao, wanatakiwa kubadilika kama tunataka ajira," alisisitiza Okash.

Mkuu wa Wilaya alisema kuwa miezi mitatu iliyopita alikaa na viongozi mbalimbali wa viwanda na kujadiliana njia ya kuongeza ajira rasmi na zisizo rasmi kwenye maeneo yao.

"Kwa sasa tubasubiri watakapoanza mchakato huo, watatupatia taarifa na tayari tumeanza na kata ya Lugoba ambayo tumepeleka majina ya vijana ili wananchi wajitokeze wa maeneo hayo ya karibu kwa ajili ya kufanyiwa usajili muda utakapofika," alisema.

Pia alisema ajira zinazotolewa zinazingatia vigezo, kama hauna vigezo huwezi kulazimisha mwajiri uajiriwe, hivyo wananchi wazingatie suala hilo.

Akielezea utekelezaji wa Ilani ya CCM, Mkuu wa Wilaya alisema katika kipindi cha miezi sita, wilaya hiyo imepokea zaidi ya Sh. bilioni 11 kwa ajili ya utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri za Chalinze na Bagamoyo.

Okash alisema fedha hizo ni kutoka Serikali Kuu, halmashauri (Mapato ya ndani) na wadau wa maendeleo ambao wamewezesha utekelezaji miradi ya maendeleo ikiwamo sekta za elimu, afya, maji, kilimo, mifugo, nishati na barabara.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bagamoyo, AbdulSharifu Zahoro aliwataka wanachama kijiandaa kwa ajili ya uchaguzi ujao kwa kuwa na wawakilishi bora watakaopeperusha bendera ya chama hicho.

Pia alisisitiza madiwani na viongozi wa chama hicho kufuatilia miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao na kutoa taarifa pale wanapobaini kuwa na tatizo ili litatuliwe mapema.

# 30 mbaroni tuhuma kutaka kupata mafao ya wizi NSSF

**Na Maulid Mmbaga**

WATU 30 wamekamatwa kwa tuhuma za kughushi nyaraka mbalimbali za udanganyifu wa taarifa za vifo, ugonjwa na kustaafu zilizolenga kuibia Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), baadhi yao wakiwa ni watumishi wa taasisi za kifedha.

Akizungumzia sakata hilo jana, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema kuwa kwa kushirikiana na maofisa wa shirika hilo walikamata watuhumiwa hao kwa nyakati tofauti kati ya Desemba 2023 na Aprili mwaka huu.

Alisema watuhumiwa hao wamekamatwa na nyaraka za bandia zinazohusu kuacha kazi, vyeti vya huduma, taarifa za uongo za ugonjwa, hati za uongo za kufukuzwa kazi na fomu za kughushi za kuomba mafao ya NSSF.

"Waliokamatwa ni pamoja na Diocress Kahwa (35), mkazi wa Mbezi na Mwalimu wa Shule ya Msingi ya Maxmilian ya Segerea jijini; Barnabas Bonivencha na wenzake 11 wa kampuni binafsi ya ulinzi ya G4S waliowasilisha taarifa za uongo za kuacha kazi ili wapate mafao wakati bado wako kazini.

"Wengine ni Gregory Rweikiza (44), mkazi wa Goba; na Carolina Mushi (37), mkazi wa Upanga, Ilala na mtumishi wa Benki ya Stanbink ambao wana tuhuma za kughushi taarifa za hospitali za ugonjwa ili wapate fao la matibabu," alisema Muliro.

Pia wamo Michael Mpogolo (38) na Sabato Thomas (27), wakazi wa Madale Mivumoni, Dar es Salaam wenye tuhuma za kughushi nyaraka za wafanyakazi wawili waliofariki dunia ambao ni Servas Tesha na Korodias Shoo waliokuwa wanafanya kazi katika Mgodi wa Geita Gold Mining (GGML).

"Watuhumiwa wote watafikishwa makahamani haraka iwezekanavyo kujibu tuhuma zinazowakabili, Jeshi la Polisi linawataka watu waachane na mambo ya udanganyifu au kughushi nyaraka kwa kuwa watakamatwa na kuchukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani kwa hatua za kisheria," alisisitiza.

### MAKOSA YA JINAI

Kamanda Muliro (pichani) pia alisema katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam liliwafikisha mahakamani watuhumiwa mbalimbali, akiwamo Joshua Saidi wa Kinondoni ambaye amehukumiwa kifungo cha maisha baada ya kupatikana na hatia ya kulawiti na kubaka.




Pia alitaja washtakiwa wengine wawili Karmal Mohamed na Mfaume Hassan wa Kigamboni na Ukonga, mtawalia, ambao wamehukumiwa kifungo cha maisha baada ya kupatikana na hatia ya makosa ya kutenda kinyume cha maumbile.

Mshtakiwa mwingine ni Justine Kasera wa Kinondoni ambaye amehukumiwa kifungo cha miaka 60 kwa tuhuma za kubaka na kulawiti, Meshack Michael wa Kinondoni amehukumiwa miaka 50 kwa tuhuma za kubaka, Babu Ally Mwinyinvua wa Mburahati na wengine wanne wamehukumiwa vifungo vya miaka 30 kila mmoja baada ya kupatikana na hatia ya kubaka.

"Mashauri mengine yapo katiki hatua mbalimbali za kusikilizwa. Tunawaomba wananchi wafike mahakamani kutoa ushahidi," alisema.

Kamanda Muliro alipoulizwa na mwandishi wa gazeti hili kuhusu kifo cha mwanasheria aliyeuawa katika mgogoro wa ardhi uliotokea hivi karibuni eneo la Tegeta, alisema uchunguzi unaendelea.

### MAKOSA BARABARANI

Kamanda Muliro pia alibainisha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, kulikuwa na makosa 221,724 ya usalama barabarani yaliyothibitishwa na polisi. Kati yake, 173,190 yanahusisha magari na 48,534 pikipiki.

Alisema kuwa hatua za kisheria zimechukuliwa ikiwamo kupigwa faini za papo hapo na baadhi ya madereva wamefikishwa mahakamani.

Alibainisha kuwa madereva wa pikipiki na magari waliofikishwa mahakamani ni 89, waliokamatwa kwa ulevi na kupigwa faini ni 60, waliokamatwa kwa kupita taa nyekundu na kupigwa faini papo hapo 759, waendesha pikipiki waliozidisha abiria (mishikaki) ni 3,779 pamoja na makosa mengineyo 217,034.

"Kuhusu sherehe za sikukuu ya Eid el Fitri, madereva wa vyombo vya moto wote wanaelekezwa kutotumia vileo wakati wa kuedesha magari na pikipiki kwani kutafanyika ukaguzi wa kushtukiza na watakaobainika sheria itachukua mkondo wake. Pia wazazi wanakumbushwa kuepuka kuwaacha watoto wadogo kutoka peke yao barabarani na maeneo mengine.

"Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha usalama unaimarishwa katika maeneo yote ya Dar es Salaam, zikiwamo nyumba za ibada, mitaani, fukwe za bahari na katika makazi ya watu. Jeshi linawatakia kila la kheri katika sikukuu hiyo," alihitimisha Kamanda Muliro.


halotel

**TAARIFA KWA UMMA**

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano inayoendelea kuboresha huduma na kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga simu na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama zetu za makato pindi mteja atakapokuwa hajajiunga kwenye kifurushi.

**GHARAMA ZA NDANI YA NCHI**

| Kipengele | Gharama |
|---|---|
| Kupiga Halotel kwenda Halotel | 10 Tsh/Dk |
| Kupiga Halotel kwenda mitandao mingine | 20 Tsh/Dk |
| Kutuma SMS | 5 Tsh/SMS |
| Data (MB) | 9.35 Tsh/MB |

**GHARAMA ZA NJE YA NCHI**

GHARAMA ZA KUPIGA SIMU NJE YA NCHI

| Kanda | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| **Ukanda 1:** USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| **Ukanda 2:** Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| **Ukanda 3:** Rwanda, Afrika Kusini, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| **Ukanda 4:** Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| **Ukanda 5:** Burundi | 1,350 |
| **Ukanda 6:** Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| **Ukanda 7:** Mitandao ya satelite | 13,800 |

GHARAMA ZA KUTUMA SMS NJE YA NCHI

| SMS | Gharama |
|---|---|
| SMS kwenda nje ya nchi | 95 Tsh/SMS |

| Aina ya kifurushi | Muda | Gharama (Tsh) | Mitadao Yote (Dk) | Halotel-Halotel (Dk) | SMS | Data (MB) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| VIFURUSHI VYA SAUTI | | | | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 350 | 25 | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | | 110 | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | 60 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku | 1,000 | 180 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku 2 | 1,000 | 160 | | 25 | |
| Dakika & SMS | Siku | 700 | 10 | Kila Dk 5 za mwanzo bure | | |
| Dakika & SMS | Wiki | 1,500 | 180 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 2,500 | 350 | 50 | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 3,000 | 450 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 4,000 | 400 | 50 | 50 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 5,000 | 550 | 650 | 100 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 10,000 | 1,600 | 1,600 | 150 | |
| Dakika & SMS | Bila Kikomo | 500 | 20 | | | |
| VIFURUSHI VYA SMS | | | | | | |
| SMS | Siku | 100 | | | 200 | |
| SMS | Wiki | 500 | | | 2000 | |
| SMS | Mwezi | 1,000 | | | 10,000 | |
| VIFURUSHI VYA INTANETI | | | | | | |
| Intaneti | Siku | 350 | | | | 170 |
| Intaneti | Siku | 500 | | | | 245 |
| Intaneti | Siku | 1,000 | | | | 490 |
| Intaneti | Siku | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Siku 10 | 2,100 | | | | 1024 |
| Intaneti | Wiki | 1,000 | | | | 490 |
| Intaneti | Wiki | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Wiki | 3,000 | | | | 1475 |
| Intaneti | Wiki | 5,000 | | | | 2460 |
| Intaneti | Wiki | 10,000 | | | | 4925 |
| Intaneti | Mwezi | 10,000 | | | | 4920 |
| Intaneti | Mwezi | 20,000 | | | | 9850 |
| Intaneti | Mwezi | 30,000 | | | | 14780 |
| Intaneti | Mwezi | 50,000 | | | | 24600 |
| VIFURUSHI VYA COMBO | | | | | | |
| Combo | Wiki | 2,000 | 55 | | 20 | 850 |
| Combo | Wiki | 2,500 | 20 | | 20 | 1150 |
| Combo | Wiki | 3,000 | 100 | | 30 | 1250 |
| Combo | Siku 10 | 3,100 | 150 | 20 | 300 | 1024 |
| Combo | Mwezi | 10,000 | 280 | | 50 | 4000 |
| Combo | Mwezi | 20,000 | 400 | | 100 | 8500 |
| Combo | Mwezi | 50,000 | 600 | | 200 | 22000 |

Halotel Tanzania Halotel_Tanzania

www.halotel.co.tz

*Vigezo na masharti kuzingatiwa

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio hiki kikokotoo mafao ya wastaafu kifike mwisho

**KILIO** cha kikokotoo cha mafao kwa wastaafu kimeendelea kusikika kila kona kutoka kwa wafanyakazi kupitia vyama vyao na vyama vya siasa.

Kwa sasa kimegusa wabunge ambao ndio waliopitisha sheria hiyo ambayo kwa sasa inaonekana kuwa kandamizi kwa wastaafu. Wabunge hao waliochangia hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 24/25, wameinyooshea serikali kuwa ni kiini cha tatizo hilo.

Wabunge hao wamesema tatizo hilo kwa sasa ni kubwa tofauti na ahadi iliyotolewa na serikali kuwa wafanyakazi wameboreshewa mafao. Kinyume chake, walisema kikokotoo hicho kina madhara makubwa kwa wastaafu, hivyo ni vyema kamati ikaundwa ili kupata ufumbuzi wa haraka.

Mmoja wa wabunge hao, Mrisho Gambo (Arusha Mjini - CCM), wakati akichangia hotuba ya makadirio hayo, pamoja na kushauri kuwapo suluhu ya jambo hilo, alisema kuna kilio cha wafanyakazi kila kona.

Alisema katika uchunguzi wake kwa miaka 10 iliyopita, amebaini kwamba kikokotoo cha zamani kilikuwa bora kuliko cha sasa na hicho ndicho Watanzania wengi wanakitaka.

Kwa mujibu wa kikokotoo hicho, mfanyakazi anapostaafu alikuwa anachukua asilimia 50 ya mafao yake na kuendelea kupata mafao kwa miaka 15.5.

Kikokotoo cha sasa mfanyakazi anapostaafu anapata mafao ya mkupuo asilimia 33 na kuendelea kulipwa kwa miaka 12.5 tu. Pia kikokotoo hicho kimepunguzwa kutoka 1/540 na sasa ni 1/580 na kimechukua wastani wa mshahara wa miaka mitatu iliyo bora badala ya 10 iliyokuwa katika kile cha awali.

Kutokana na mfumo huo mpya wa ukokotoaji mafao, mbunge huyo amekwenda hatua zaidi, amebaini kuwa kwa kikotoo cha awali cha zilizokuwa PSSF ma LAPF, mfanyakazi aliyekuwa akilipwa mshahara wa Sh. 800,000 kwa mwezi alikuwa anapata mafao ya mkupuo ya Sh. 57,466,666 na kwa kikokotoo cha sasa ni Sh. 28,675,862.

Pamoja na kuwapo kwa tofauti hiyo ya Sh. 29,190,804 mfanyakazi wa sasa anayestaafu anapata Sh. 388,137 badala ya Sh. 401,000 ya malipo ya kila mwezi.

Kutokana na ukweli huo na bila kuuma maneno, mbunge huyo aliweka bayana kwamba katika hali ya kawaida kwenye kikokotoo hicho, yamefanyika makosa makubwa ambayo kwa sasa yanaumiza wafanyakazi ndiyo maana wameamua kuwatumia wabunge kwa kuwa ndio waliopitisha.

Hoja hiyo kwa nyakati tofauti, imeungwa mkono na wabunge wengi wakiwamo Ester Bulaya (Viti Maalumu - CHADEMA), Issay Paulo (Mbulu Mjini CCM) na Nicodemus Maganga (Mbogwe - CCM) ambao licha ya kueleza kuwa wanapokea ujumbe kutoka kwa wastaafu kuhusu maumivu ya kikokotoo hicho, wamesisitiza kurudi katika meza ya mazungumzo na vyama vya wafanyakazi kukipitia upya.


Wahenga wanasema mwenye uchungu ni aliyefikwa na janga. Msemo huo unasadifu kilio cha kikokotoo kwa wastaafu baada ya kuonja shubiri baada ya kupokea mafao hayo.

Jambo lingine linalotia uchungu ni baadhi ya kauli za viongozi wa serikali kwamba lengo la kikokotoo hicho ni kuwatunzia fedha wastaafu kwa madai kuwa wanaweza kutumia vibaya na kupata taabu baadaye. Serikali inapaswa kutambua kwamba wafanyakazi hao wametumika kwa zaidi ya miaka 30 hadi 40 na wanahitaji kufaidi matunda yao ya utumishi.

Kuna msemo kwamba kuteleza si kuanguka, hivyo ni vyema serikali irejee mezani na vyama vya wafanyakazi ili kuona njia nzuri ya kurekebisha jambo hilo na hatimaye kuwafuta uchungu wa moyoni wafanyakazi hawa ambao wamelitumikia taifa kwa uaminifu mkubwa. Ni vyema kilio hiki sasa kikafika mwisho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kwa darasa hili, wanasiasa wanaweza kujifunza kitu kutoka kwa Dk. Nchimbi

**KATIKA** uwanja wa siasa baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi, kumekuwapo sintofahamu inayotokana na baadhi ya wanasiasa kuchukiana kwa sababu za itikadi tofauti.

Mtindo huo unawafanya warushiane maneno makali, bila ya kutambua kuwa siasa sio chuki wala uadui, bali tofauti ya itikadi, lengo ni moja la kujenga nchi yao Tanzania.

Wakati hali ikiwa hivyo, kwa baadhi ya wanasiasa, lakini upande wa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi ni kinyume, kwani kiongozi huyo anasema haonei haya urafiki kati yake na sehemu kubwa ya viongozi wa vyama vya upinzani.

Mwanasiasa huyo anafafanua kuwa hawezi kujivunia Utanzania wake kama hana mapenzi na Watanzania wenzake na kwamba itikadi za vyama haziwezi kukwaza urafiki wake na watu.

Hilo ni katika kongamano la Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, lililoandaliwa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Dar es Salaam juzi.

Anajenga hoja kuwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, wakati wa uhai wake aliwapenda Watanzania wote bila kuwabagua na kwamba hata yeye haoni haya kuwa na urafiki na viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani.

Dk. Nchimbi anasema, amekuwa akiwasiliana nao kila wanapoonekana wamezungumza vibaya katika mikutano ya hadhara.

Kwa maelezo hayo, ninadhani wanasiasa wana la kujifunza kutoka kwa kiongozi huyo, upinzani wa kisiasa haupaswi kuwafanya wachukiane bali waendeshe siasa huku wakiweka utanzania wao mbele.

Dk. Nchimbi anasisitiza kuwa, misingi ya Utanzania ni kuwapenda Watanzania wengine, bila ya kufikiria ubaguzi wa kiitikadi, rangi wala kabila. Binafsi ninakubaliana naye kwa asilimia 100.

Ninadhani wanasiasa wote wakiwa na mtazamo kama wake, hakutakuwa na kushambuliana kwa maneno wala kuchukiana bali wataweka Utanzania mbele katika harakati zao za kisiasa.

Iwapo mfano wa mwanasiasa huyo utaigwa, ninaamini hakutakuwa na kauli kwamba sehemu ya wapinzani, serikali haiwezi kupeleka maendeleo, huku wakisahau kuwa maendeleo hayana chama.

Kushindana kwa hoja zenye mashiko ni jambo zuri zinatoa nafasi viongozi kujitafakari na kuchukua hatua badala ya kuchukiana, hivyo wanasiasa ni vyema wasichukie wala kufanyiana 'mtimanyongo'.

Hivyo, kwa maelezo hayo ya Dk. Nchimbi, upinzani sio uadui, na kwamba hakuna sababu ya msingi ya kugombana wenyewe kwa wenyewe bali washindane kwa hoja kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Ni wazi wanasiasa wanaochukiana au kugombana watakuwa wameishiwa hoja, hivyo ni vyema wakajifunza jambo kutoka kwa mwanasiasa huyo ambaye ameonyesha kutokubaliana na siasa za kuchukiana.

Iwapo mfano wa Dk. Nchimbi utazingatiwa, ninadhani kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa na hata uchaguzi mkuu hazitakuwa na sintofahamu kama ambavyo imewahi kutokea miaka ya nyuma.

Imekuwa kawaida wakati wa kampeni kukutana wafuasi wa vyama vya siasa wakishusha bendera za vyama vingine, kuvunja vijiwe na hata kutishiana kwa maneno badala kushindana kwa hoja za kujenga nchi.

Lakini, ninadhani wakijielekeza kwenye Utanzania wao na kuachana na chuki zinazotokana na itikadi za kisiasa kama alivyo Dk. Nchimbi, itakuwa rahisi kushirikiana kuleta maendeleo.

Wawe ni wafuasi wa vyama vya; CCM, CUF, CHADEMA, ACT- Wazalendo na vingine, wote wangetambuana kama Watanzania, badala ya kuegemea kwenye itikadi za kisiasa ambazo kwa namna moja au nyingine, zinaweza kukwamisha nchi kupiga hatua kwenda mbele.

Kitendo cha mwanasiasa au wanasiasa kutamka hadharani kuwa serikali haiwezi kupeleka maendeleo sehemu inayoongozwa na upinzani, hiyo inaweza kuwa ni chuki ya wazi badala kutengeneza urafiki kama Watanzania. Wanasiasa mngejifunza kutoka kwa Dk. Nchimbi.

# Bilioni 1.3/- zatolewa kukabili mafuriko

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 1.3 kwa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro kutekeleza miradi ya dharua ya ujenzi wa mifereji ya kisasa, miundombinu ya barabara za vijiji na kuboresha kingo za mito ili kumaliza tatizo la mafuriko ya mara kwa mara yanayotokea katika wilaya hiyo kongwe kihistoria.

Akizungumza wakati wa ukaguzi na kutembelea miradi hiyo, akiongozana na Kamati ya Siasa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya, Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema tayari serikali imetoa fedha kusaidia kuimarisha miundombinu ambayo awali ilikuwa haipo na kusababisha maji kuingia kwenye nyumba za wananchi na kusababisha mafuriko.

Prof. Kabudi alipongeza hatua hiyo ya serikali ya kutoa fedha hizo na kwamba sasa itakuwa mkombozi kwa wakazi wa Kilosa kwa kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wanaathiriwa na mafuriko hayo hata pale mvua zisiponyesha katika wilaya hiyo na kunyesha mikoa mingine kutokana na mito mingi kupita katika wilaya hiyo.

"Kwa moyo wa dhati kabisa, ninashukuru serikali kwa kutupatia fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ikiwamo mifereji ya kisasa kabisa, hii itatusaidia kuondokana na hali ya mafuriko," alisema Prof. Kabudi.

Alisema jiografia ya Mji wa Kilosa imezungukwa na milima na mito mikubwa, hivyo imekuwa vigumu kuepukana na mafuriko tangu enzi za wakoloni, hivyo ujenzi wa miundombinu hiyo utasaidia kumaliza tatizo hilo la mafuriko.

"Sasa historia inakwenda kuandikwa baada ya serikali kutenga zaidi ya Sh. bilioni 1.3 ili kujenga mifereji ya kisasa katika maeneo hatarishi," alisema.

Akizungumzia mkakati wa wilaya hiyo kuondokana na mafuriko hayo, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara wa Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Kilosa, Wiston Munyaga, alisema fedha hizo zitajenga mifereji ili kuondoa adha ya maji yanayotokana na mito mbalimbali inayosababisha mafuriko.

Diwani wa Mvumi, wilayani Kilosa, Shaban Malingo, alisema mafuriko yanayotokea wilayani mwao yamekuwa yanagharimu maisha ya watu na makazi.

## Wafanya utafiti kutambua wanawake mashujaa nchini

**Na Restuta James**

CHUO cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kimeanza utafiti kutambua mchango wa wanawake mashujaa wa Tanzania walioshiriki harakati mbalimbali za kujenga nchi kuanzia za kupinga ukoloni na kudai uhuru.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam juzi, Mkuu wa Idara ya Stadi za Jinsia katika chuo hicho, Dk. Sarah Mwakyambiki, alisema utafiti huo ulianza miaka minne iliyopita na tayari wametambua wanawake 63 ambao mchango wao katika harakati za ujenzi wa taifa haujatambuliwa.

Dk. Sarah alisema kati ya wanawake 63 waliowapata, 59 ndio historia zao zimekamilika na wanne hazijakamilika.

Alisema yupo aliyeshiriki Vita vya Majimaji, ambaye alikuwa mwanamke pekee aliyenyongwa usiku mweusi kutokana na kwamba alikuwa mstari wa mbele kutoa taarifa za kinachoendelea kwenye ngome ya wakoloni.

Alisema mwanamke mwingine ni rubani na injinia wa ndege ambaye alikuwa anahudumia na kutengeneza ndege ya Rais na za viongozi wakuu wa nchi wanaotembelea Tanzania.

Alisema mwanamke mwingine ni aliyehamasisha harakati za siasa na kupanda mizizi ya CCM hadi ngazi ya shina na ndiye aliyekuwa anazungumza kabla Mwalimu Nyerere hajahutubia mikutano mingi. Mwanamke mwingine ni hakimu wa kwanza na mwingine ni aliyefanikiwa kusimamia hoja ya kuondoa kodi ya kiti.

"Kuna mama ambaye alitoa jengo lake kuipa CCM, limekuwa ofisi za chama miaka mingi iliyopita, wapo wasanii na wataalamu wa ustawi wa jamii," alisema.

Dk. Sarah alisema miongoni mwa wanawake hao, yupo pia ambaye alikuwa Mwafrika na Mtanzania wa kwanza kufanya kazi katika Ikulu ya Tanzania.

"Tunaona sasa hivi mtu anaweza akatoa, akafanya jambo kwa kuwa kuna vyombo vya habari na mitandao akaonekana yeye ni wa kwanza wakati kuna watu wamewahi kufanya huko nyuma, lakini rekodi zao hazizungumzwi popote," alisema.

Katika utafiti huo, wamepitia nyaraka na magazeti kuanzia ya mwaka 1965 na kufanya mazungumzo na ndugu au wahusika waliopo hai ili kuweka kumbukumbu za utumishi na utendaji wao vizuri.

Utafiti umewaweka wanawake hao katika makundi 12, likiwamo la harakati za kupinga ukoloni, kudai uhuru, elimu, uongozi kitaifa, kimataifa, utumishi wa umma, majeshi, sekta binafsi na michango katika jamii. Umekamilika, unasubiri fedha kuchapishwa.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together we can build a better life)

**PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES**

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER**

| S/N | DESCRIPTION | | FEES AND CHARGES TZS | USD |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Monthly Maintanance | SA | 2,000.00 | 2 |
| | | CA | 6,000.00 | 4 |
| 2 | Non Maintanance of Minimum Balance | SA | 1,500.00 | 2 |
| | | CA | 4,000.00 | 4 |
| 3 | Account Statement Charges | SA-Monthly | - | 0 |
| | | SA-Interim | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| | | CA-Monthly | Free | Free |
| | | CA-Interim | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| 4 | Cash withdrawal | SA-Up 25M | Free | |
| | | SA-Over 25M | 0.26% | |
| | | SA-Up to $2K | | Free |
| | | SA-$2K-$5K | | 0.60% |
| | | SA-Over $5k | | 0.60% |
| | | CA-Up to 25 M | Free | |
| | | CA-Above 25M | 0.26% | |
| | | CA-Up to USD 5K | | Free |
| | | CA-$ 5K-$10K | | 0.60% |
| | | CA-Above $ 10K | | 0.60% |
| 5 | Cash Deposit Charges | SA-Up to 25M | Free | |
| | | SA-Over 25M | 0.22% | |
| | | SA-Up $5K | | Free |
| | | SA-Over $5K | | 0.50% |
| | | SA-small currency ($1 to $20) | | 10.00% Minimum charge $1 |
| | | CA-Up to 50M | Free | |
| | | CA-Over 50M | 0.22% | |
| | | CA-Up to $10K | | Free |
| | | CA-Over $10K | | 0.50% |
| | | CA-small currency ($1 to $20) | | 10.00% Minimum charge $1 |
| 6 | Balance Confirmation Certificate | SA | 12,800.00 | 10 |
| | | CA | 21,200.00 | 13 |
| 7 | Account Closure Charges | SA | 20,000.00 | 20 |
| | | CA | 50,000.00 | 50 |
| 8 | Activation of Dormant Account | SA | Free | Free |
| | | CA | Free | Free |
| 9 | Stop Payment Charges | SA | Free | Free |
| | | CA | 35,000.00 | 28 |
| 10 | Cheque Return Charges/Dishonoured Cheque | CA-Inward | 50,000.00 | 50 |
| | | CA-Outward | 50,000.00 | 50 |
| 11 | Cheque Clearing Charges | CA-Inward | 1,300.00 | 1 |
| | | CA-Outward | Free | Free |
| 12 | Ledger folio charges per folio (40lines per | SA | Free | Free |
| | | CA | 6,000.00 | 4.00 |
| 13 | Cheque book Charges | CA-50 Leaves | 42,000.00 | 27 |
| 14 | Mobile Banking | | | |
| i | Withdrawal Charge | Upto 100,000 | 1,700.00 | N/A |
| | | 101,000 to 200,000 | 2,600.00 | N/A |
| | | 201,000 to 400,000 | 4,300.00 | N/A |
| | | 401,000 to 600,000 | 5,100.00 | N/A |
| | | 601,000 to 999,000 | 6,800.00 | N/A |
| ii | Funds Transfer/Mobile Wallet | Upto 100,000 | 500.00 | N/A |
| | | 101,000 to 250,000 | 900.00 | N/A |
| | | 251,000 to 500,000 | 1,700.00 | N/A |
| | | 501,000 to 1,000,000 | 4,300.00 | N/A |
| | | 1,001,000 TO 10 Mn | 8,500.00 | N/A |
| 15 | Locker Rent-Yearly | Small | 296,700.00 | N/A |
| | | Medium | 508,500.00 | N/A |
| | | Big | 635,600.00 | N/A |
| 16 | Remittances | | | |
| i | TISS | Any amount per 1 | TZS 8,450.00 | TZS 8,450.00 Equivallent |
| ii | E Remittances | Upto USD 1000 or Eq. TZS | 17,000.00 | $ 9.00 |
| | | 1001 to 5000 | 20,400.00 | $ 11.00 |
| | | 5001 to 10000 | 40,700.00 | $ 22.00 |
| | | 10,001 and above | 84,800.00 | $ 43.00 |
| iii | Swift Outward | Upto 5,000 | NA | $ 39.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 51.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 77.00 |
| iv | Swift Inward | Upto 5,000 | NA | $ 11.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 16.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 26.00 |

| S/N | DESCRIPTION | | FEES AND CHARGES TZS | USD |
|---|---|---|---|---|
| 17 | Loan/Advances Related Charges | | | |
| i | Processing Charges | Upto 5 Mio - | 21,200.00 | |
| | | 5Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | |
| | | 10 Mio to 25mio - | 339,000.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | |
| | | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | |
| | | Upto 5,000 - | | $85.00 |
| | | 5000 to 10,000 - | | $170.00 |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.28% |
| | | >500,000--* | | 1.06% |
| ii | Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | |
| | | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | |
| | | Upto 50,000 | | FREE |
| | | >50,000 - (Min 150) | | 0.26% |
| iii | Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - | 21,200.00 | |
| | | 5 Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | |
| | | 10Mio 25mio - | 381,400.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | |
| | | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.53% |
| | | >500,000--* (*minimum 9000) | | 1.28% |
| iv | Inspection Charges | Upto 100 Mio - | 21,200.00 | |
| | | >100 mio - | 42,400.00 | |
| | | Upto 50,000 | | $22.00 |
| | | >50,000 | | $43.00 |
| v | Credit Reference Report Charges | | 101,700.00 | $43.00 |
| vi | Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 2.00% | 2.00% |
| 18 | Guarantees (Local & International) | | | |
| i | Bonds & Guarantees | per quarter (Min TZS 75,000) | 1.02% | 1.02% |
| ii | Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | 0.43% |
| 19 | Letter of Credit | | | |
| 19.1 | Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof) | | | |
| i | Opening commission | commission Min $ 200 | NA | |
| ii | LC amendment Commission | Commision Min $50 max 350 | NA | 1.02% |
| iii | Swift charge for LC opening | | NA | 0.34% |
| iv | Swift charge for other message/amendments | | NA | $34.00 |
| v | Extensions - Commissions | commission Min $ 200 | NA | $34.00 |
| vi | LC cancellation charges | commission Min $ 200 | NA | 1.02% |
| vii | Non payment of Bills on due date | Till Payment | NA | 1.02% |
| 19.2 | Export Letters of Credit (per quarter or part thereof) | | | |
| i | Advising commission | | NA | $119.00 |
| ii | Confirmation Commission | Commision Min $150 | NA | 0.43% |
| iii | Negotiating bills under LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% |
| iv | Reimbursement claim paid | Commision Min $75 | NA | 0.43% |
| v | Extensions - | Commision Min $200 | NA | 1.02% |
| vi | Collection of Export LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% |
| vii | Amendments | | NA | $64.00 |
| 20 | Other disclosures | | | |
| i | Base or Prime Lending Rate | | 16% | 10% |
| ii | Maximum spread | | 5% | 5% |
| iii | Penal Interest | | | |
| | a.For non compliance on Terms of Saction | Rate per year over regular rate of interest | 3% | 3% |
| | b.For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | Rate per year over regular rate of interest | 5% | 5% |
| vi | Deposit Rates | | | |
| | a. Current account | | Nill | Nill |
| | b. Savings bank deposit | | 3.00% | 1.00% |
| | C. Fixed Deposits Rates | **Up to TZS 50 M(up to USD 50,000)** | | |
| | | 30 -90days | 3.50% | 1.50% |
| | | 91-180days | 4.50% | 2.25% |
| | | 181-364 days | 5.50% | 3.00% |
| | | 1 year and above | 8.00% | 3.75% |
| | | 2 Years and Above | 8.00% | 4.00% |
| | | **TZS 50 M-100M (USD 50,000 -USD 100,000)** | | |
| | | 30 -90days | 4.50% | 2.25% |
| | | 91-180days | 5.50% | 2.50% |
| | | 181-364 days | 7.00% | 3.50% |
| | | 1 year and above | 8.25% | 4.25% |
| | | 2 Years and Above | 9.00% | 4.75% |
| | | **Above 100 M(Above USD 100,000)** | | |
| | | 30 -90days | 5.50% | 2.50% |
| | | 91-180days | 6.50% | 3.25% |
| | | 181-364 days | 7.50% | 4.00% |
| | | 1 year and above | 8.50% | 4.75% |
| | | 2 Years and Above | 9.50% | 5.00% |

| | |
|---|---|
| HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | 08-Apr-24 |
| GM-CREDIT | 08-Apr-24 |
| HEAD BUSINESS OPERATIONS | 08-Apr-24 |

# Migogoro kifamilia chanzo watoto wanaoishi mazingira magumu

**Na Denis Mambya**

MIGOGORO ya kifamilia imetajwa sababu inayochangia ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira magumu nchini na kuwasababishia kuhama nyumbani na kuishi katika mazingira hatarishi.

Akizungumza kwa njia ya simu na gazeti hili, Ofisa Ustawi wa Jamii, Hassan Awf, kutoka Shirika la Amani Centre for Street Children lenye makao yake jijini Arusha, alisema kuwa kwa asilimia kubwa utengano baina ya wazazi huchangia watoto wengi kuishi katika mazingira hatarishi.

Awf alisema kuacha jukumu la ulezi wa wototo kwa wasaidizi wa kazi ni moja kati ya kisababishi cha watoto wengi kuhama kutoka nyumbani kutokana na ukatili wanaokumbana nao kutoka kwa wasaidizi hao kutokana na kutotimiza kikamilifu jukumu la ulezi wa watoto hao.

"Kutokuwa na biashara rafiki kwa kina mama wengi hapa nchini ni miongoni mwa sababu iliyoonesha kuwepo kwa ongezeko la watoto waishio katika mazingira magumu baada ya utengano na waume zao kwani jukumu kubwa la ulezi wa watoto hubaki mikononi mwao,hivyo kushindwa kutimiza kwa ukamilifu," alisema.

Kwa mujibu wa utafiti wa Headcount report wa mwaka 2017 uliyofanywa na Railway Children Afrika (RCA), jumla ya watoto 6,393 huwapo mitaani wakati wa mchana sawa na aslimia 76 kwa watoto wa kiume na watoto wa kike asilimia 24, wakati wa usiku jumla ya watoto 1,385 sawa na asilimia 70 kwa watoto wa kiume huku watoto wa kike ikiwa ni asilimia 30.

Mikoa iliyoongoza kwa na idadi kubwa ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na idadi yao kwenye mabano ni Dar es Salaam (3,312), Mwanza (1,254), Iringa (1,191), Mbeya (841), Arusha (673) na Dodoma (507), idadi hiyo inajumuisha nyakati zote mchana na usiku.

Fatma Mwinyimvua, mkazi wa Kata ya Bungo, Manispaa ya Morogoro, aliwashauri wazazi kuwa waangalifu kupunguza idadi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu kutokana na utengano baina yao kuathiri kwa kiasi kikubwa makuzi ya watoto hasa wa kike.

Isack Amos, mkazi wa Kata ya Bungo, Manispaa ya Morogoro, alisema wazazi wanatakiwa kuwa na uelewa mpana hasa kwa wale walio katika ndoa kudumisha upendo na amani ya ndoa kwa lengo la kuepusha madhara yatakayo wakumba watoto wazazi wanapofarakana.

Ukatili dhidi ya watoto kutoka kwa wazazi ama walezi unaelezwa kuchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira magumu nchini, taasisi za malezi zikiwamo shule na dini zimetakiwa kusimama kupambana na vitendo hivyo ili kuwanusuru watoto wa kitanzania wenye malengo na ndoto kubwa.



Wakazi wa kata ya Upanga Magharibi, jijini Dar es Salaam, wakiwa wamebeba baadhi ya vyakula walivyopewa msaada na Shirika la Smh Rail Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC), kwenye Msikiti wa Tambaza juzi, kwa ajili ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wajasiriamali wafundishwa kupata soko Afrika

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

ZAIDI wanawake 100 kutoka wilaya mbalimbali mkoani Mtwara, wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu kanuni, taratibu na sheria za kufanya biashara katika soko huru la Afrika.

Akizingumza wakati wa mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara, Nanjiva Mzunda, alisema mafunzo hayo yatawasaidia wajasiriamali namna ya kupata masoko na kuuza biashara zao.

Mafunzo hayo ni ya siku mbili yameandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC) wakidhaminiwa na Shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na masula mbalimbali ya kijamii nchini (Trade Mark East Africa).

"Mafunzo haya yatawafanya wajasiriamali hawa waweze kushindana kimataifa, katika kuuza bidhaa zao, kwahiyo nina imani wakitoka hapa watakuwa wamepikika, kuiva tayari kiushindani wa kibiashara," alisema Nanjiva.

Mkurugenzi wa Bodi ya Chama cha Wafanyabiashara Wanawake nchini (TWCC), Mwajuma Ankoni, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha wajasiriamali hao wanauza bidhaa zinazoingia katika soko la Afrika.

"Wajasiriamali hawa watafundishwa utaratibu, sheria na kanuni na namna gani bidhaa wanazozalisha zinazotakiwa ziingie katika soko la Afrika," alisema Ankoni.

Ofisa udhibiti ubora kutoka Shirika la Viwango Nchini (TBS), mkoani Mtwara Ismael Laizer, alisema wanafanya jitihada mbalimbali katika utoaji wa elimu kwa wajasiriamali wadogo kwa kupitia njia mbalimbli ikiwamo maonesho ya Nanenae ili wafahamu hatua wanazopaswa kufuata ili kupata nembo ya ubora.

# Wataalam kutafiti milima inayoporomosha mawe Rukwa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amesema serikali itapeleka wataalamu wa miamba mkoani Rukwa kufanya utafiti katika safu za milima ya Lyamba lya Ufipa eneo la kijiji cha Nkwilo, wilayani Sumbawanga ambalo mawe mengi yanaporomoka na kuharibu barabara na kubomoa nyumba za wananchi na kusababisha vifo.

Waziri Bashungwa aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mtowisa, wilayani Sumbawanga akiwa katika siku yake ya kwanza ya ziara ya kukagua miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua mkoani humo.

"Serikali inafanya kila iwezalo kuhakikisha inarejesha miundombinu ya barabara kilometa 180 inayopita katika vijiji vya Kasansa - Muze - Mtowisa - Ilemba - Kaoze - Kilyamatundu ambayo imeharibika kwa kiasi kikubwa na mvua," alisema Bashungwa.

Pia, serikali imeahidi kufanya matengenezo makubwa ya barabara katika maeneo korofi ya Nkwilo, Mtowisa, Zimba, Kisa, Kinambo, Ilemba na Solola ambayo pia yameathiriwa.

Kupelekwa kwa wataalamu hao kumekuja kutokana na kuwapo kwa changamoto ya milima kumeguka na kuporomoka na hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Nyakia Chirukile alitoa taarifa ya tukio la watu wawili wa familia moja Sai Weja (26) na Geshi Gweu (7), kupoteza maisha baada ya jabali la udongo kuporomoka kutoka mlimani na kuipiga nyumba wanayoishi.

Katika tukio hilo watu wengine 15 walijeruhiwa na eneo kutajwa kuwa hatari kwa wananchi kuendelea kuishi na kuwataka wahame ili wawe salama na familia zao.

Aidha, maporomoka ya udongo huo ni matokeo ya mvua kubwa zinazoendelea kunyesha kwenye safu za milima ya Lyamba Lya Ufipa na kufanya udongo kuloana chepe chepe na kuhifadhi maji mengi na tope linaloporomoka kutoka kwenye milima hiyo.

## Askari hifadhi misitu waonywa kujihusisha rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbasi, ameonya askari wapya wa hifadhi za misitu nchini, kutotumia nguvu au kupokea rushwa na kuacha rasilimali za umma zikiharibiwa.

Badala yake, ameelekeza wajishushe na kuhudumia wananchi katika maeneo mbalimbali ya misitu nchini, na pale wanapokosea wawaelimishe.

Dk. Abbasi alikuwa akizungumza jana na askari wa hifadhi 96 katika Chuo cha Viwanda na Misitu (FITI) kilichoko Moshi, mkoani Kilimanjaro, baada ya kuhitimu mafunzo ya awali ya uhifadhi na kuwa tayari kuanza majukumu yao kama watumishi wa umma.

"Mnakwenda kuwahudumia wananchi katika maeneo mbalimbali ya misitu nchini ni matarajio yetu mtawahudumia wananchi na pale wanapokosea kuwaelimisha;

"Badala ya kutumia nguvu au kupokea rushwa kuacha raslimali zikiharibiwa. Binafsi nikisikia hayo kwenu nitasikitika sana na tutachukua hatua kali.

"Pamoja na mambo mengine niliyowaeleza yatakayowasaidia kufika mbali suala la maadili ndio msingi mkuu.

Akiwa chuoni hapo, pia ametembelea Chuo cha Viwanda na Misitu (FITI) na kuzungumza na wafanyakazi, ambako alisema serikali inakijali chuo hicho na inayo mipango ya kukiboresha.

"Wizara imeanza mpango wa uboreshaji wa chuo hiki cha FITI, ikiwemo kuongezewa bajeti kwa zaidi ya asilimia 100 katika mwaka wa fedha utakaoanza Julai mwaka huu."

**"Badala ya kutumia nguvu au kupokea rushwa kuacha raslimali zikiharibiwa. Binafsi nikisikia hayo kwenu nitasikitika sana na tutachukua hatua kali.**

# Upungufu wa wataalam wa uzalishaji mbegu waathiri

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

UPUNGUFU wa wataalam wa uzalishaji wa mbegu za mboga, unatishia uhai wa mbegu hizo katika nchi nyingi za Bara la Afrika ikiwamo Tanzania, hivyo kuzifanya kuwa tegemezi wa mbegu kutoka Asia na Ulaya.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la World Vegetable Centre katika Bara la Afrika, Dk. Gabriel Rugalema, alisema kwa sasa mazao ya mboga za kiafrika hayapatikani kwa wingi, kwa sababu hakuna mtafiti anayezishughulikia.

Akizungumza jana na wataalam 15 wa utafiti kutoka Shirika la Utafiti wa Kilimo la Serikali ya Uganda (NARO) katika makao makuu ya shirika hilo yaliyoko Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, Dk, Rugalema alisema:

"Kwa hiyo serikali ya Uganda, imeamua pamoja na mazao mengine wanataka kwenda kwa kina kwenye uzalishaji wa mbegu mpya na bora katika mazao ya mboga; na wanataka wataalamu wao wawe na utaalam wa kina.

"Sasa ukiangalia utaalam wa kina watautapata wapi zaidi ya nchi za Asia na Ulaya, kituo kilichoko peke yake hapa Afrika ni WVC (World Vegetable Centre). Mafunzo yanachukua wiki moja na yanaangalia uzalishaji kwa ujumla, kuanzia vinasaba unavichaguaje mpaka unapata mbegu bora.

...Je, ukishaipata mbegu bora inazalishwaje kwa wingi, tunaita seeds multiplications. Halafu ikitoka hapo inaendaje kwa yule ambaye ataipitisha iwe mbegu ya kibiashara (seeds certification) na ikitoka hapo itakwendaje sasa sokoni."

Kituo cha World Vegetable Centre kimekuwa kikihusika na ukusanyaji, uchambuzi, upembuzi na uboreshaji wa mboga za asili dunia nzima kwa zaidi ya miaka 20.

Benki ya mbegu iliyoko Tanzania, ndiyo ya kwanza kwa ukubwa Barani Afrika, ikihifadhi mbegu za asili ambazo ndio rasilimali muhimu katika uboreshaji wa mazao palipo na mabadiliko ya tabianchi.

Ofisa Mfawidhi wa Kanda ya Kaskazini wa Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Munguatosha Ngomuo, kwa mujibu wa NARO, kwa miaka miwili sasa soko la mbegu la Uganda, limekua kutoka dola milioni tatu hadi dola milioni 50, jambo limewashtua Waganda na kuona kumbe iko haja ya wao kuanza kuchukua hatua ya kudhibiti biashara ya mbegu.

"NARO imepiga kambi WVC ili kujengewa uwezo kwa ujumla wa namna bora ya kudhibiti biashara ya mbegu, uagizaji na uingizaji lakini pia uzalishaji wa mbegu nchini mwao.

"Kwa maelezo ya watalam hao wa Uganda, kule kwao sekta ya mboga na matunda, hasa mbegu bado iko chini, kwa sababu hawana sheria na kanuni zinazowawezesha kudhibiti ubora, uingizaji na uagizaji wa mbegu za mboga na matunda.

...Lakini pia hata breeding programs zao (uzalishaji wa mazao) bado iko chini sana. Kwa hiyo wamekuja hapa ili waweze kujengewa uwezo wa namna ya kuanzisha breeding programu ya mazao ya mboga lakini pia jinsi ya kuendesha shughuli ya kudhibiti huo ubora wa mbegu za mboga na matunda kwa nchi ya Uganda.

Kitu kikubwa kinachowavutia hawa ni regional harmonization kama za Afrika ya Mashariki na SADC, kwani wanajifunza jinsi ambavyo kupitia hizi harmonization wanaona ni sehemu ya biashara kubwa ya mbegu katika ukanda wa Afrika ya Mashariki."

Jopo hilo la wataalamu wa mazao ya matunda na mboga kutoka nchini Uganda, linaongozwa Dk. Gabriel Ddamulira, ambaye ni Ofisa Mkuu wa Utafiti wa NARO.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (wapili kulia), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi wa kampuni ya Franone Mining Ltd, Onesmo Mbise kwa kusaidia jamii inayowazunguka katika Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro juzi. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga na (wa tatu kulia), ni Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tuhuma uhujumu mali AICC zang'oa maofisa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TUHUMA za uhujumu na wizi wa mali za umma katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) zilizoibuliwa na Bunge, hatimaye zimewang'oa wakurugenzi watatu na maofisa waandamizi wa kituo hicho kupisha uchunguzi.

Waliosimamishwa kazi ni Mkurugenzi wa Fedha na Utawala, Savo Mung'ong'o, Mkurugenzi wa Mikutano na Masoko, Mkunde Mushi na Mkurugenzi wa Miliki na Miradi, Victor Kamagenge.

Wengine ni Mhasibu Mkuu, Augustine Karadoga, Mkuu wa Rasilimali Watu na Utawala Festo Mramba na Meneja wa Kituo cha Mikutano kilichoko Jijini Dar es Salaam (JNICC), Catherine Kilinda.

Jana, Mkuu wa Kitego cha Mawasiliano cha AICC, Freddy Maro, alithibitisha kuwa watumishi hao sita, wamesimamishwa ili kupisha uchunguzi, na kwamba taratibu na hatua nyingine kuhusu uchunguzi huo zitatolewa baadae kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Uchunguzi huo unaanza, ikiwa ni siku cahche, tangu Rais Samia Suluhu Hassan, amteue Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kituo hicho, Christine Mwakatobe, Machi 18 mwaka huu.


Februari 9, mwaka huu, Bunge liliibua hujuma hizo na wizi na kutoa baraka za kukamatwa, kuchunguzwa na kuchukuliwa hatua, baadhi ya watumishi wanaokihujumu Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), kwa kushiriki kuuza viwanja na mali za umma, kinyume na utaratibu.

Aidha, baadhi ya maeneo ya kituo hicho cha diplomasia ya mikutano, ambacho hutumika kutangaza nchi kimataifa na kuvutia wageni, yamevamiwa na kujengwa miundombinu ya kudumu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa, alilieleza Bunge kuwa, AICC pamoja na mchango wake kwa uchumi wa nchi, baadhi ya watumishi wameshiriki kuuza mali za kituo, ikiwamo viwanja.

Kawawa alisema kutokana na hujuma hizo, Bunge limeazimia hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi waliohusika na wanaohusika wa kituo hicho; na watakaobainika kushiriki uuzaji wa viwanja na mali za kituo kinyume na taratibu wawajibike.

Vilevile, Bunge liliazimia hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watu wote waliovamia na watakaovamia viwanja vya kituo hicho cha mikutano cha kimataifa cha AICC.





# NCU yakabidhiwa bilioni 1.8/- akaunti maalum

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SERIKALI ya Mkoa wa Mwanza imekikabidhi Chama Kikuu Cha Ushirika Nyanza (NCU 1984), zaidi ya Sh. bilioni 1.8 zilizokuwa zimehifadhiwa katika akaunti maalum.

Akizungumza jana jijini hapa katika hafla ya makabidhiano ya fedha hizo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda alisema, fedha zilikuwa zimehifadhiwa katika akaunti hiyo iliyofunguliwa mwaka 2018.

Alisema fedha hizo zaidi ya Sh.bilioni 1.8 zilitokana na makusanyo ya mali mbalimbali za NCU 1984, zilizorejeshwa na serikali kutoka kwa watu waliokuwa wakizimiliki kinyume na utaratibu.

"Baada ya kurejeshwa kwa mali hizo, Ofisi ya Waziri Mkuu iliyokuwa ikiratibu ilielekeza kufunguliwa kwa akaunti maalum iliyokuwa ikisimamiwa na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kwa kipindi cha mpito, wakati mchakato wa kurejesha umiliki wa mali hizo kwa NCU ukiendelea," alisema Mtanda.

Alisema, kwa kipindi chote serikali ya mkoa ilikuwa ikisimamia akaunti hiyo maalum ya NCU 1984 hadi Aprili 5, mwaka huu, ilikuwa na salio la zaidi ya Sh. bilioni 1.858 nao mkoa una matumaini fedha hizo zitatumika kukiimarisha chama hicho na wanachama wake.

Naibu Mrajisi wa Vyama Vya Ushirika wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) Collens Nyakunga, kwa niaba ya Mrajisi Mkuu wa Ushirika alisema, NCU 1984, ilikuwa ikidaiwa na Benki ya CRDB Sh. bilioni 2, lakini benki hiyo ilichukua mali zilizozidi fedha ilizokuwa ikidai.

Alisema CRDB walichukua mali ya bilioni 16 wakati deni ni Shilingi bilioni mbili na serikali ilibaini mali tisa zilizokuwa zikimilikiwa na NCU zilitaifishwa bila utaratibu, zikiwamo za kiwanda cha New Era Oil Mill, jengo la KAUMA, Kiwanda cha Mkonge na viwanja vyake vitatu.

"Pia kuna kiwanda cha Ashok na viwanja vyake 12, ghorofa ya kuishi na nyumba nyingine zilizopo Isamilo, hivyo mali zilizorejeshwa zina thamani ya Sh. bilioni 61.3," alisema Nyakunga.




Mkurugenzi wa Shirika la WEADO, Eliasenya Nnko akizungumza na baadhi ya viongozi na makundi mbalimbali ya kijamii katika kata ya Lyabukande, wilayani Shinyanga juzi, kuhusu kuondokana na mila kandamizi zinazochochea ukatili wa kijinsia kama mimba, ndoa za utotoni na vipigo kwa wanawake. **PICHA:MARCO MADUHU**

## Shule mahitaji maalum zaomba kukumbukwa

**Na Remmy Moka,** SAUT

SERIKALI na wadau wameombwa kuzitazama shule zenye mahitaji maalum ili kuhakikisha wanafunzi wa shule hizo wanapata huduma stahiki kama wanafunzi wengine.

Rai hiyo ilitolewa na Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Mitindo iliyopo wilayani Magu, mkoani Mwanza, January Guze baada ya kupokea msaada wa magodoro 16, madawati 20 na fimbo kwa wanafunzi wasioona kutoka kwa wanafunzi wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IMF) ndaki ya Mwanza.

Alisema shule hiyo inakabiliwa na ongezeko kubwa la wanafunzi na mahitaji yakiwa mengi ikiwamo miuondombinu ya kujifunzia sio rafiki na kutokidhi idadi ya wanafunzi wenye uhitaji maalum katika shule hiyo.

Viviani Msofe, mmoja wa wanafunzi waliotembelea na kutoa misaada kwa shule hiyo alisema lengo lao ni kutatua baadhi ya matatizo yanayowakabili wanafunzi hao pia aliwaomba wadau mbalimbali zikiwemo taasisi zinazohusika na watoto wenye ulemavu wa ngozi kuwatembelea wanafunzi hao mara kwa mara kwani wanaitaji uangalizi na huduma zinazopatikana kwa wakati ili afya zao zizidi kuwa imara na waweze kuzingatia masomo ipasavyo.

"Tunaiomba serikali, taasisi za umma na binafsi kuweka nguvu kubwa katika shule hiyo na shule zingine za watu wenye uitaji kwani hakuna kitu kizuri kama kutazama kizazi kijacho kwa mtazamo mpana lengo la kufanya hivyo ni kubadirisha maisha na kurahisisha mazingira ya kujifunzia ili wanafunzi hao waweze kupata mahitaji muhimu ya kimasomo na afya zao

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walitoa shukrani zao kwa wanachuo hao na kuziomba taasisi zingine kuwatazama kwa jicho la tatu kwani wanahitaji kushikwa mkono ili waweze kupata afya njema na elimu stahiki.

# Wawekezaji walia ubovu barabara Msalala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAWEKEZAJI wa ndani sekta ya madini Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameiangukia serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) kuhakikisha wanatengeneza miundombinu ya barabara ili kupata urahisi wa kusafirisha madini wanayoyapata hadi sokoni.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa kiwanda cha kuchakata madini ya dhahabu (Plant) cha Sojem Investment, Sonda Joseph, wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama Mboni Mhita ya kusikiliza na kututa kero mbalimbali zinazowakabili ili kuongeza uzalishaji na serikali kupata mapato yake, kilichopo kijiji cha Kalole kata ya Lunguya Msalala.

Alisema, wanahofu ya kupoteza mzigo wawapo safarini kutokana na barabara kuwa mbovu huo kutoka katika eneo lao hadi sokoni inawafanya kuchukua muda mrefu kufika na wakati mwingine wanakuta muda wa soko umekwisha na kulazimika kulala na dhahabu katika nyumba za kulala wageni, hatua ambayo inawatia hofu ya kupoteza mali wanazozalisha.

"Hivi karibuni nilikuwa na kilo 12 za dhahabu nilikuwa nazipeleka sokoni, lakini kwa ubovu wa barabara nilifika muda wa soko ukiwa umeisha na kulazimika kulala na dhahabu nyumba za kulala wageni, ingepoteza serikali ingepoteza zaidi ya Sh. milioni 70 hivyo tunaiomba serikali kututengenezea miundombinu ya barabara," alisisitiza.

Naye Mwenyekiti wa kikundi cha Shangaza Gold Mine Menani Sanga alisema, kuna barabara inayotumika na wananchi wa vijiji vinavyowazunguka kupita katikati ya mgodi huo na wameshaandika barua TARURA kuomba kuhamishwa kwa barabara hiyo ili kupata usalama wa mali zao na mpaka sasa hakuna majibu waliyopata.

Aidha, aliomba kupewa eneo lingine kwa ajili ya kuhifadhi takataka zinazozalishwa kwani eneo hilo linamiamba mingi ambayo haina madini hivyo wanakosa sehemu ya kuyahifadhi na kurundikana sehemu moja na kuahidi kuwa wazalendo na kutojihusisha na utoroshaji wa madini ili serikali izidi kupaya kodi yake.

Mhita alisema, barabara nyingi zimeharibiwa na mvua ya masika inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali na ndio sababu ya kuzunguka maeneo yote akiwa ameambatana na maaofisa wa TARURA ili wakati wa kiangazi watambue ni maeneo gani wanahitaji kufanya marekebisho.

Alisema, serikali imekuwa mstari wa mbele kutengeneza mazingira wezeshaji ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje kwa kujenga miundombinu ya barabara, nishati ya umeme na maji ili rasilimali hiyo iweze kunufaisha wawekezaji na wananchi hasa kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye jamii.



Ukurasa 12

**Dawa za kulevya zilipofikia kupenya kubomoa maisha kwa sayansi ya juu**



Ukurasa 13

**KENGELE UCHAGUZI MITAA....**

Wanawake na kampeni yao 'Mwezeshe Ashinde' wachangishana 200/- kila siku



Ukurasa 14

**KANGANA RAUNAT**

**Kashfa kula nyama ng'ombe yamweka njia panda azma kujitosa uchaguzi siasa**



MIAKA 30 YA MAUAJI KIMBARI...

# Siku Rais Dk. Samia alipotia mguu jijini Kigali, kukumbuka ya historia

**Na Mwandishi Wetu**

WIKI hii, Rwanda taifa jirani la Afrika Mashariki, liliadhimisha kumbukumbu ya mauaji ya kimbari nchini humo.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni miongoni mwa waliohudhuria, wakiwapo viongozi wengine wa mataifa kama; Salva Kiir wa Sudan Kusini), Cyril Ramaphosa (Afrika Kusini), Petr Pavel (Jamhuri ya Czech), Andry Rajoelina (Madagascar), Mohamed Ould Ghazouani wa Mauritania na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed.

Ni tukio ambalo limebakia kuwa alama ya kitaifa, kilele chake kikiwa siku ya Aprili 7, ambayo Rais Dk. Samia alipata fursa ya kutoa heshima, mara baada ya kuweka shada la maua kwenye eneo la makaburi ya kumbukumbu ya mauaji ya Kimbari, jijini Kigali.

Pia, wakikusanyika na wakuu wa nchi wenzake wakashuhudia kuwashwa mwenge wakati wa kumbukumbu ya mauaji hayo ya Kimbari, sasa ikitimu miaka 30.

Baadhi ya viongozi wa nchi na serikali waliohudhuria kumbukumbu ya mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi wa Rwanda iliyopita wamesema hadi sasa, licha ya kubainika kuwa ulimwengu ulishindwa kuzuia mauaji hayo, bado dunia haijajifunza kutokana na kilichotokea wakati huo.

Ni kati ya kauli zilizotolewa mjini Kigali Rwanda katika mwanzo wa juma la kuadhimisha kumbukumbu za tukio hilo lenye umri miongo mitatu sasa, likiondoa uhai wa watu 800,000.

Wawakilishi wa Umoja wa Ulaya (EU) pamoja na Mwakilishi wa Umoja wa Afrika (AU), wote



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na viongozi wenzake wa kitaifa, wakishuhudia, Rais Paul Kagame, akiwasha mwenge wa kumbukumbu ya mauaji ya kimbari, jijini Kigali wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

wamekiri kwamba jamii ya kimataifa ilishindwa kusimama na kuzuia mauaji hayo licha ya taarifa za kile kilichotarajiwa kutokea.

Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya, Charles Michel na raia wa Ubelgiji nchi iliyopoteza walinda amani wake 10 nchini Rwanda katika mauaji hayo, akatamka:

"Nasikitishwa na mzizi wa historia hii, pia nikiwa na aibu mimi kama raia wa Ubelgiji na mtu kutoka Bara la Ulaya, ambalo likuwa na uwezo pamoja na nchi yangu, lakini sote tulishindwa kufanya lolote kuyasimamisha mauaji haya."

Pia, wiki hii jijini hapo Kigali, kulikuwapo viongozi ngazi za manaibu rais, waziri wakuu, viongozi wa mashirika mbalimbali ya kimataifa na viongozi wengine waandamizi kutoka mabara Ulaya, Afrika, Asia na kwingineko.

Vilevile lilikuwapo Shirika la kimataifa linalowakilisha Jumuiya ya Wayahudi la World Jewish Congress (WJC),katika nchi 100 kwenye Serikali, mabunge na mashirika ya kimataifa,

Rais Paul Kagame akihutubia kwenye tukio la kumbukumbu lililofanyika katika ukumbi wa BK Arena jijini Kigali, huku baadhi ya viongozi wakihoji dunia ilishindwa kuyazuia mauaji hayo

Rais Kagame katika ufafanuzi wake, akasema mzizi wa tatizo ukachukua sura katika ukanda wa nchi za maziwa makuu, pale wanamgambo wa Kihutu wa FDLR waliofanya mauaji hayo walipokimbia.

**SAMIA JIJINI KIGALI**

Ziara hiyo ya Rais Dk. Samia jijini Kigali si ya kwanza na hata binafsi amekuwa mwenyeji huko. Akiwa na miezi kadhaa ya urais, Dk. Samia, akiboresha uhusiano wa nchi na majirani wa EAC, mnamo Agosti mwaka 2021, alizuru jijini Kigali kukutana na mwenyeji wake, Rais Kagame, lengo likitajwa kuimarisha uhusiano wao.

Iliripotiwa kwamba, siku ya kwanza wakuu hao wa nchi walikuwa na mazungumzo binafsi na siku iliyofuata, wakajumuika na walioambatana nao.

Ni katika ziara ambayo Rais Dk. Samia, pia akazuru eneo la mauaji ya kimbari ya mwaka 1994, ambako nako katika ziara hiyo akatoa heshima yake.

Zao la ziara hiyo kukashuhudiwa kutiwa saini makubaliano ya kushirikiana katika mambo manne, ikiwamo; Habari, Mawasiliano, Teknolojia, Uhamiaji, Elimu, Tiba ya Binadamu na bidhaa zake.

Rais Kagame akanukuliwa, akitamka katika hotuba yake: "Rwanda na Tanzania, ushirikiano wao ni zaidi ya mipaka. Ushirikiano wetu wa kina na utashi wetu kusogeza umeme kwa watu wetu uko juu"

Hapo akafafanua mbali, kuhusu uhusiano katika Jumuiya ya AfrikaMashariki, kwamba majibu yake yanapatikana kupitia ushirikiano na hasa kwenye kuchangia fursa, kwa kila upande.

**INAENDELEA UK. 14**

# Dawa za kulevya zilipofikia kupenya kubomoa maisha kwa sayansi ya juu

**Na Zanura Mollel**

UHALIFU mtandaoni ni miongoni mwa Matukio yanayopangwa na kuvuka mipaka ikishirikisha magenge makubwa ya kihalifu na yenye nguvu kifedha kwa kuhusisha eneo wanakokusudia a kutenda jinai, mfani ndani ya nchi.

Ni shughuli za jinai zinazofanyika kupitia mtandao unaogawanyika katika aina tofauti, ikiwamo wizi wa kimtandao, udanganyifu wa mtandaoni (phishing), ulaghai wa kadi za mkopo, utapeli mtandaoni, unyanyasaji mtandaoni (cyberbullying), ukiukaji wa faragha mtandaoni (cyberstalking) pamoja na biashara haramu mtandaoni.

Uhalifu mtandaoni ni shughuli za kihalifu zinazofanywa kupitia mtandao wa kompyuta au vifaa vya kidigitali. Kukua kwa teknolojia na matumizi ya Tekniliojia ya Mawasiliano na Habari (TEHAMA), kumeanza kuchangia matendo hayo kufanyika ikihusisha biashara haramu kwa njia ya digitali kwa kuhusisha uuzwaji na usafirishaji wa dawa za kulevya, ambazo nchini Tanzania haziruhusiwi.

Dawa za kulevya, ni kemikali au vitu vingine vinavyotumiwa kwa lengo la kulevya. Biashara haramu ya dawa za kulevya kwa njia ya mtandao inahusisha mauzo, ununuzi, na usafirishaji wa dawa za kulevya kupitia mtandao.

Wafanyabiashara hao hutumia mitandao ya giza (dark web) au mitandao ya kijamii kufanya biashara haramu, pasipo kujulikana. Wanaweza kutumia mifumo ya kryptografia na njia zingine za kuficha utambulisho wao.

Mitandao ya giza; ni sehemu za mtandao ambazo hazipatikani kwa urahisi kupitia injini za utafutaji za kawaida kama mtandao wa 'Google Search.

Sehemu hizo za mtandao zinajulikana kwa utata na shughuli haramu kama vile biashara ya dawa za kulevya, silaha, na huduma nyinginezo zisizofaa kisheria, wanaotumia mitandao hiyo mara nyingi hutumia teknolojia iitwayo 'kryptografia' ili kuficha shughuli zao.

**MAMLAKA DCEA**

Taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) tarehe 04, mwezi huu, inasema Dawa mpya ya Kulevya iliyotambulika kwa jina la Methylene Dioxy Pyrovalerone (MDPV) kilo 4.623 ilikamatwa mjini Dar es salaam.

Taarifa inaeleza kuwa, dawa hiyo ipo katika kundi la vichangamshi na hutengenezwa kwa kutumia kemikali bashirifu ambayo huweza kuleta madhara ya haraka kwa mtumiaji, msafirishaji aliyenaswa akiwa raia wa Comoro, mwenye umri miaka 32.

Ni biashara inayofanyika kwa



Shamba la dawa za kulevya lililobainika hivi karibuni katikati ya Msitu wa Ubangu, mkoani Tabora, ikifyekwa. **PICHA: MTANDAO**

> "Pia, zaidi ya uzito au ujazo ulioainishwa katika kifungu cha 15A adhabu yake ni Kifungo cha Maisha jela. Kifungu cha 29(1)(c) kinaainisha uzito wa kilo 30 yabisi au lita 30 kimiminika au zaidi...

njia ya mtandao wa intaneti na kusafirishwa kwa kutumia kampuni za usafirishaji mizigo nchini, zikiwa kwenye vifungashio venye chapa za majina bandia kama vile mbolea na kadhalika.

**UN VS UHALIFU**

Alipohutubia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa siku ya Alhamisi Desemba 7,2023, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres akasema hatua zaidi zinahitajika kukabiliana na changamoto inayoongezeka kila kuchao, uhalifu uliopangwa ambao unafanyika kimataifa, kuvuka mipaka ya kitaifa.

Uhalifu unaofanywa kimataifa inaingizaa mabilioni ya Dola za Marekani, ambazo nchini zina thamani ya shilingi trilioni kadhaa, ikihusisha biashara haramu ya dawa za kulevya, utoroshaji wa fedha, biashara haramu ya silaha, usafirishaji haramu wa binadamu, usafirishaji haramu wa maliasili na bidhaa nyingine, vyote ambavyo vina uhusiano.

"Ingawa ni katika aina tofauti tofauti,madhara yake yanafanana kudhoofisha utawala, ufisadi na ukosefu wa sheria, ghasia kufanyika kwa uwazi, vifo na uharibifu,"anasema Guterres.

Anaeleza uhalifu huo huchochea vurugu na mizozo akitolea mfano wa uhalifu wa kupangwa wa kimataifa katika maeneo mbalimbali duniani kama vile Afghanistan na Colombia, ambako uzalishaji wa dawa za kulevya na usafirishaji vimechochea mizozo ya kikatili na ya muda mrefu.

Amegusia pia nchini Haiti, kulikonaswa katika hatihati ya kuporomoka kwa serikali, kuchochea uhalifu wa magenge na unaongezeka iashara haramu ya silaha zinazongizwa nchini humo.

Katibu Mkuu anasema, iwezezesha magenge kudhibiti miundombinu kama vile bandari na hata barabara kuu, shughuli za makundi yanayohusika na uhalifu wa kimataifa na makundi yalivojihami zinaendana, ivyo kufanya harakati za kumaliza mizozo kuwa ngumu.

Guterres anasema, kuna uhusiano kati ya uhalifu wa kupangwa kimataifa na ugaidi, jambo analosema linatia hofu, akitoa mfano Ukanda wa Sahel barani Afrika, biashara haramu ya mafuta, dawa za kulevya, silaha na maliasili, inawezesha makundi yaliyojihami kupata silaha na kutishia maisha ya wananchi na mbinu zao za kujipatia kipato.

**UNODC**

Mkuu wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuzuia Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani, (UNODC), Ghada Waly,a anasema makundi hayo yamejipanga zaidi na yamefika hatua ya kuwa na wataalamu.

Hapo anafafanua: "Tunahitaji taasisi zenye uwezo wa kutoa haki na kumaliza ukwepaji sheria, pamoja na jamii zenye mnepo.

"Tunahitaji kuwekeza rasilimali zaidi ili kukabili masoko haramu yenye thamani ya matrilioni ya dola," anasema Ghada.

**KEMIKALI BASHIRIFU(GCLA)**

Ofisa Kemikali bashirifu Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Kanda ya Kaskazini(DCEA) Cosmas Mhesa, anasema matumizi halali ya kemikali ni uzalishaji mali kama vile Dawa, shughuli za ,aabara, matumzi viwanda vya nguo, vipodozi, rangi, uchenjuaji wa madini pamoja na kutumika katika tafiti mbalimbali.

"Madhara ya kemikali hizo hutokea pindi zinapochepushwa kwenda kwa wahalifu na kutumika katika matumizi haramu ikiwemo kutengeneza dawa za kulevya pamoja na kutengeneza silaha au vilipuzi," anasema Mhesa.

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Sura Namba 5 ya mwaka 2015 Sura 95 maboresho ya mwaka 2019, kifungu cha 15(b) na 15A kinazuia kufanya yafuatayo kinyume cha sheria Kumiliki kemikali bashirifu, kusafirisha kemikali bashirifu, kuchepusha kemikali bashirifu,Kutengeneza kemikali bashirifu,Kujihusisha kwa namna yeyote na kemikali bashirifu.

"Kifungu cha (15 na 15A) pamoja na kuzuia, kimeainisha makosa na adhabu kwa watakaobainika kukutwa na kosa linalohusisha kemikali bashirifu kiasi cha lita 100 kimiminika (Liquid Form), kilo 100 yabisi(Solid Form) au chini ya kiwango kilichotajwa hapo adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela.

"Pia, zaidi ya uzito au ujazo ulioainishwa katika kifungu cha 15A adhabu yake ni Kifungo cha Maisha jela. Kifungu cha 29(1) (c) kinaainisha uzito wa kilo 30 yabisi au lita 30 kimiminika au zaidi, mshtakiwa hatoweza kupata dhamana," anasema Mhesa.

Anafafanua, kukua kwa sayansi na teknolojia duniani, Wahalifu wamefikia hatua ya kutumia kemikali bashirifu peke yake kuzalisha dawa mpya za kulevya zenye nguvu zaidi ya dawa zilizozoeleka na shughuli zao hufanyika kwa kificho sana kupitia maabara bubu (Clandestine Laboratories)".

**KAMISHNA LYIMO**

Kamishna Jenerali Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Aretas Lyimo anasema kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2023, namlaka hiyo ilidhibiti kilo 157,738.55 za kemikali bashirifu zilizokuwa zikiingizwa nchini kinyume na sheria ambazo zingeweza kutumika kutengeneza dawa za Kulevya.

Taarifa ya Dawa za Kulevya Mwaka 2022 ilieleza kiasi Tani 98.29 na Lita 85 za kemikali bashirifu zilizuiliwa kuingizwa nchini, kwa kuwa hazikukidhi matakwa ya kisheria za nchi na kimataifa pia ilibaini usafirishaji haramu wa kemikali hiyo lita 25,000 na baadhi ya kampuni kufanya biashra bila usajili.

KENGELE UCHAGUZI MITAA...

# Wanawake na kampeni yao 'Mwezeshe Ashinde' wachangishana 200/- kila siku

• Lengo kuongeza idadi yao wanaojitosa katika uongozi

**Na Sabato Kasika**

MWAKA huu ni wa uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, ambao baadaye utafuatiwa na uchaguzi mkuu wa Rais wabunge na madiwani utakaofanyika mwaka ujao.

Wakati uchaguzi wa viongozi wa mitaa, vijiji na vitongoji ukitarajiwa kufanyika mwaka huu, baadhi ya wanawake nao wameanza mikakati yao kuwezeshana kuwania uongozi katika uchaguzi huo.

Katika harakati hizo, wanawake wajasiriamali 86 wa Kata ya Kipunguni Dar es Salaam, wameanzisha umoja wao ili kufanya kampeni waliyoipa jina la 'Mwezeshe Ashinde', wakimaanisha kumwezesha mwanamke.

Wiki iliyopita wanawake hao walikutana, katika ofisi za Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni kuweka mikakati ya kufanikisha kampeni yao hiyo huku pia wakichagua uongozi wa kufanikisha lengo lao.

Aliyechaguliwa kuwa mwenyekiti wa umoja huo, Maria Mushumbusi, anayesema uchaguzi unahitaji fedha na kufafanua kuwa wanawake wengi hawana uwezo kiuchumi, hivyo ni vyema wasaidiwe.

"Hivyo, tumeona tuanzishe kampeni hii, ili kuwaunga mkono wenzetu watakaojitokeza kuwania uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuwachangia fedha za kampeni," anasema Mary.

Mama huyo anafafanua, hatua waliyoichukua ya kuanzisha kampeni ya 'Mwezeshe Ashinde', itasaidia pia kuwaepusha wanawake kuingia katika vishawishi vya kutaka watoe rushwa ya ngono ili kupata nafasi za uongozi.

"Unajua huwa kuna tuhuma kwamba baadhi ya wanawake wanaoonyesha nia ya kutaka kuwania uongozi huombwa rushwa ya ngono, sababu kubwa ni kwamba hawana uwezo kiuchumi, sasa tumeona kuna haja ya kuwawezesha wenzetu kiuchumi waepuke rushwa hiyo," anasema.

**KAMPENI ILIVYO**

Mary akifafanua hilo, anasema katika kufanikisha kampeni yao kinamama, wamekubaliana kila mmoja kuchangia Sh.200 kila siku, kwa muda wa miezi minne kuanzia Mei hadi mwazoni mwa Septemba.

"Tumekubaliana kukutana Aprili 16 ili kufungua akaunti ya Mkoba ambayo tutatumia kuweka michango ya fedha itakayotumika kuwezeshana katika uchaguzi wa serikali za mitaa," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, baada ya kufungua akaunti wajasiriamali hao wataanza kudunduliza fedha katika akaunti hiyo kuanzia Mei Mosi hadi Septemba 2 mwaka huu.

"Kila mjasiriamali atakuwa anaweka akiba ya Sh. 200 kwa siku, hivyo katika kipindi hicho cha miezi minne tunatarajia kukusanya Sh. milioni 2,064,000, hata kama hazitatosha, lakini huo ni mwanzo, tutaendelea kujipanga zaidi kwa uchaguzi mkuu," anafafanua.

Anasema, wameamua kuelekeza nguvu zao kwenye uchaguzi huo, kwa maelezo kwamba, ofisi nyingi za serikali za mitaa zikiwa na viongozi wengi wanawake, vitendo vya ukatili ndani ya jamii vitapungua.

"Wanawake ni watu wenye huruma, hivyo wakiwa wengi kwenye uongozi wanaweza kusimamia kikamilifu vita dhidi ya vitendo hivyo, hivyo wito wangu ni kwamba tuanze kuwashawishi wenzetu wenye uwezo wa kuongoza wajiandae kuchukua fomu," anasema.

Mary anawataka wale ambao hawana vyama wajiunge katika vyama, kutokana na kwamba utaratibu uliopo wa kupata nafasi za uongozi kuanzia serikali za mitaa hadi Rais, ni lazima mgombea awe na chama.

Aidha, anasema wakati wa uandikishaji wapigakura katika daftari la kudumu la wapigakura, watahamasisha wanawake wajiandikishe kwa wingi ili baadaye wawaunge mkono wenzao watakaowania uongozi.

Katibu wa umoja huo, Mama Zainabu Omary, anasema wamefikia hatua hiyo baada ya kuunganishwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, na kwamba itakuwa rahisi kwao kupaza sauti zao kwa pamoja.

"Awali kila mtu alikuwa kivyake, lakini kupitia umoja huu tuliouanzisha, vitu vingi ikiwamo mfuko wa kusaidia, akaunti ya pamoja, tunapeana mikopo midogo midogo," anasema Zainabu.

Zainabu anasema, wameshapata mafunzo ya kupambana na vitendo vya ukatili, ikiwamo rushwa ya ngono, ukeketaji, ndoa za utotoni na haki nyingine za wanawake.

Mhazini wa umoja huo, Tausi Msangi anawahamasisha, wakati wa kujiandikisha ukifika watapita nyumba kwa nyumba kuhamasisha wanawake wote wanajiandikishe kwenye daftari la kudumu la mpigakura.

"Vilevile, tunatarajia kuhamasisha wanawake wengine wajiunge na kampeni hii, ili kila mwanamke awaunge mkono wanawake watakaopitishwa kuwania uongozi wa Serikali za Mitaa," alisema Tausi.

**UCHAGUZI ULIOPITA**

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Seleman Bishagazi, anakariri ripoti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopita, kati ya nafasi 62,612 za wenyeviti wa vitongoji, wanawake walioshinda ni 4,171 tu.

"Kwa mujibu wa NEC, idadi hiyo ni sawa na asilimia 6.7, hiyo ndiyo hali halisi ya ushiriki wa wanawake katika uongozi, wakati umefika wa kuwekeza ili kuongeza nafasi za wanawake wa kuchaguliwa viongozi katika ngazi za vijiji, vitongoji na mitaa," anasema Bishagazi.

Kwa upande wa madiwani, anasema taarifa ya NEC, uchaguzi wa mwaka 2020, inaonyesha kuwa ushiriki wa wanawake katika mabaraza ya madiwani, wanawake wa kuchaguliwa kutoka kata 260, kati ya madiwani 3,952 sawa na asilimia 6.58, madiwani wa viti maalum ni 1,374.

"Hao ni kutoka halmashauri zote, sawa na asilimia 24.59 ya madiwani wote nchini. Kwa ujumla, madiwani wanawake ni 1,634 kati ya madiwani wote 5,587 sawa na asilimia 29.24. Upande wa wenyeviti wa halmashauri zote 185, wanawake ni watano na meya mmoja," anasema.

Aidha, anatolea mfano sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, katika mkoa wa Dar es Salaam kuwa inakadiriwa kuwa na watu 5,383, 728, huku asilimia 52 wakiwa ni wanawake.

"Cha kushangaza ni kwamba, kuanzia uchaguzi wa mwaka 1965 hadi 2020, jumla ya mameya 10 walichaguliwa jijini Dar es Salaam, hakuna meya mwanamke hadi sasa, kwa takwimu hizo, ushiriki wa wanawake katika vyombo vya uwakilishi bado ni mdogo," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, hali hiyo hailingani na azma ya kimataifa ya kufikia uwiano sawa wa kijinsia na maendeleo endelevu ifikapo mwaka 2030, katika vyombo vyote vya maamuzi.



Mary Mushumbusi (mbele), akizungumza kwenye mkutano wa kinamama kujitosa uchaguzi mitaa. **PICHA: SABATO KASIKA**

> Vilevile, tunatarajia kuhamasisha wanawake wengine wajiunge na kampeni hii, ili kila mwanamke awaunge mkono wanawake watakaopitishwa kuwania uongozi wa Serikali za Mitaa.

JUKWAA LA VIONGOZI

KANGANA RAUNAT

# Kashfa kula nyama ng'ombe yamweka njia panda azma kujitosa uchaguzi siasa

Na Mwandishi Wetu

MUIGIZAJI wa India aliyejitosa katika siasa akiwania kuteuliwa kuwa mgombea wa chama tawala, akilazimika kukanusha uvumi kuwa anakula nyama ya ng'ombe, ambayo ni kinyume na imani, pia mila zao.

Kangana Ranaut, mfuasi mkubwa wa chama cha Bharatiya Janata (BJP), amekanusha akijihami kwa kauli kutoka kwa wapinzani wake kwamba "(madai) ya aibu" na "uvumi usio na msingi".

Suala la ulaji wa nyama ya ng'ombe ni nyeti sana nchini India, kwani katika badahi ya jamii ng'ombe wanachukuliwa kuwa 'Watakatifu; ikiabudiwa na kubwa katika jamii hiyo.

India, pia inatajwa kuwa nchi yenye watu wengi zaidi duniani sasa ikiipita China kuwa na watu bilioni 1.43.

Wanasiasa wengine wa chama BJP na wafuasi wa kisiasa, sasa wameshinikiza kupigwa marufuku uchinjaji wa ng'ombe.

Ranaut, mwigizaji nyota wa Bollywood ambaye ameshiriki katika baadhi ya filamu zilizoingiza pesa nyingi zaidi nchini India, amejibu baada ya mwanasiasa wa upinzani kudai kwamba hapo, awali alikula nyama ya ng'ombe.

Watumiaji kadhaa wa mitandao ya kijamii walimshutumu wakisema madai hayo yanaweza kumdhuru muigizaji huyo, ambaye anatafuta kuingia rasmi katika kuwania uongozi wa kisiasa katika wiki zijazo, akiwa mgombeaji wa chama BJP katika jimbo la Kaskazini la Himachal Pradesh.

Akiandika kwenye mtandao wa X, zamani ukijulikana kama Twitter, Ranaur akasema: "Situmii nyama ya ng'ombe au aina nyingine yoyote ya nyama nyekundu.

"Ni aibu kwamba uvumi usio na msingi unaenezwa kunihusu, nimekuwa nikitetea na kuendeleza yoga na tiba ya asili ya Ayurvedic. kwa miongo kadhaa sasa mbinu kama hizi hazitafanikiwa kuniharibia sifa.

"Watu wangu wananijua na wanajua kuwa mimi najivunia kuwa Mhindu na hakuna kinachoweza kuwapotosha."



Muigizaji Kangana Ranaut. **PICHA: MTANDAO**

> Watu wangu wananijua na wanajua kuwa mimi najivunia kuwa Mhindu na hakuna kinachoweza kuwapotosha.

### SUALA LA UCHINJAJI

Mwaka 2015, Polisi nchini India iliwakamata watu wawili kuhusiana na mauaji ya mtu mmoja wa Imani tofauti, kutokana na uvumi kwamba familia yake imekuwa ikihifadhi na kula nyama.

Mohammad Akhlaqa, alibebwa kutoka nyumbani kwake viungani mwa mji wa Delhi na kupigwa hadi kufa mapema, huku mwanawe wa kiume pia akijeruhiwa.

Mara moja, polisi ikawakamata watu wanane kuhusiana na mkasa huo, huku nayo familia ya Akhlaq ikisema ilikuwa imeweka nyama ya kondoo katika jokofui lao la ndani.

Uchinjaji ng'ombe umepigwa marufuku katika majimbo mengi ya India, kwa kuwa mnyama huyo huchukuliwa kuwa 'Mtakatifu' na idadi kubwa ya raia wa Kihindi.

Waziri Mkuu nchini India, wakati huo akakosolewa kwa kuwa kimya kuhusu tukio hilo.

Katika tukio lingine mwaka 2016, kuna wanafunzi wanne katika jimbo la Kashmir nchini India walipigwa kwa 'kupika nyama ya ngombe.

Ni mkasa mwigine, uliotokea katika chuo kimoja binfasi, badaa ya kuenea uvumi kwamba walikuwa wakipika nyama ya ngombe katika chumba chao cha kulala.

Polisi wakalazimika kuingilia kati kuwanusuru.Ni ndani ya mwaka huo, jimboni Pradesh waliwakamata wanandoa wawili wa umani tofauti waliokuwa wakisafiri kwa treni, baada ya kuwashuku kwamba walikuwa wamebeba nyama ya ngombe.

Aprili 2016, mwanamke nchini India, akiwa na binamu yake mwenye umri miaka 14, walibakwa na genge la watu wanne, ambao pia waliwaua kwa tuhuma kula nyama ya ng'ombe.

Mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 20, alisema walifanya uvamizi huo katika makazi yao jimbo la Haryana Kaskazini wiki mbili zilizopita.

"Pamoja na utetezi wetu kuwa hatukula nyama hiyo, walinibaka mimi na binamu yangu, kisha kumuua mjomba na shangazi yangu," msichana huyo ambaye jina lake limehifadhiwa akaisema.

Waumini wengi wa dini ya.... (jina lihahigfadhiwa) huwahesabu ng'ombe kuwa watakatifu na kuchinja wanyama hao kumepigwa marufuku katika majimbo mengi likiwamo Haryana.

Ni mkasa uliozua kisa ghadhabu katika jamii za eneo hilo, wahusika kisheria wakikamatwa na kushitakiwa kwa makosa yanayohusu ubakaji na mauaji.

Mewat, ni wilaya iliyo umbali kilomita 100 kutoka mji mkuu wa Delhi, hivi karibuni iliteka vyombo vya habari baada ya ofisa wa cheo cha juu, kuwaambia wanahabari kuwa polisi wangeanza kukagua chakula cha biriani kuhakikisha hakina nyama ya ng'ombe.

---

## Siku Rais Dk. Samia alipotia mguu jijini Kigali, kukumbuka ya historia

**INATOKA UK. 11**

Ndivyo mara nyingine mwaka jana Rais Dk. Samia akiwa katika tukio lingine la mjumuiko wa siasa- uchumi, alipewa fursa ya kuhutubia akakumbusha mataifa ya Kiafrika kujitahidi kuandika historia yao na kuanika vipaumbele vyake na si kuandikiwa.

Alikuwa kwenye mkutano wa Baraza la Kitalii duniani uitwao "Global Summit of the World Travel and Tourism" uliofanyika jijini Kigali.

Rais Dk. Samia akasema, mataifa ya Kiafrika yanapaswa kujiuliza maswali magumu kuhusu utalii wake, ikigusa maeneo kama ya masoko ya kimkakati, kuwa na nembo yake, pia zikitafiti na kuhifadhi mahitaji na rasilimali muhimu, ikipiga hatua ndefu.

Akafafanua, Afrika inapaswa kuhadithia historia yake na kuelezea yaliyo chanya kwa Afrika. Haipaswi kubaki kimya pale inapobebeshwa upotoshwaji juu yake.

Mtazamo wake ni kwa bara hilo kunyanyuka kujitetea katika safari ya kuunda ubora wake kule inakoenda

### ALAMA YA KUMBUKUMBU

Ni wiki hii tukio lililotawaliwa na ushuhuda wa kusononesha, likivuta hisia za wengi, hasa kutoka kwa walionusurika mauaji hayo.

Ayinkamiye Louse, aliyenusurika mauaji hayo akiwa na umri wa miaka 11, anasema yeye ni miongoni mwa mamia ya Watutsi waliokimbilia katika kanisa la Nyange wilayani Ngororero Kusini mwa Rwanda na baadaye kanisa hilo likavunjwa na kundi kubwa likauawawa.

"Ilitolewa amri ya (mtu muhimu kanisani)...kuhakikisha jengo zima la kanisa tulipokuwa tumekimbilia linabomolewa na kuwekwa chini, ili ahakikishe watutsi wote waliokuwa wamekimbia wanauawa, kanisa lilivunjwa na maisha ya ndugu wote yakaishia hapo," anasimulia.

Ni shuhuda ambazo zilionekana kuwafanya baadhi ya watu kudondosha machozi na kujawa na simanzi usoni kulingana na uzito wake

Mataifa kama ya Nigeria, Jamhuri ya Zcech na News Zealand, zimepongezwa kwa mara nyingine kutokana na ujasiri wa mabalozi wao katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kusimama na kukemea, huku wakitaja kilichokuwa kikiendelea Rwanda yalikuwa ni mauaji ya kimbari.

- **Makala hii imeandaliwa kutokana na taarifa mbalimbali zinazohusu tukio hilo la wiki hii na historia yake.**





## MBT kuinua wachimbaji wanawake, vijana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, amesema ili kuinua wachimbani madini wanawake na vijana nchini serikali itatekeleza programu ya Mining for a Brighter Tomorrow (MBT) kufikia azma hiyo.

Mavunde, alisema hayo jana jijini hapa alipofungua mkutano wa Baraza la Wafanyanyakazi wa wizara na taasisi zake na kutumia fursa hiyo kuwaagiza viongozi na watumishi wa wizara kuwa wabunifu kila wakati wanapotekeleza majukumu yao.

"Serikali ya awamu ya sita chini ya Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuimarisha wizara ya madini kwa kuitengea fedha za kutekeleza miradi na mipango mbalimbali.

"Mpango mahsusi tunao kuja nao sasa ni kuwaendeleza wachimbaji wakinamama na vijana kupitia programu ya Mining for a Brighter Tomorrow yenye lengo la kuwapatia leseni za maeneo ya uchimbaji, magari,vifaa na mitambo ya uchimbaji," alisema.

Kadhalika, alisema kupitia programu hiyo itasaidia kuchochea ukuaji wa sekta ya madini, uchumi wa taifa na kuongeza ajira kwa Watanzania.

"Tumieni hili Baraza la Wafanyakazi kuhakikisha mnakuja na mpango mzuri wa kusimamia utekelezaji wa mipango na miradi chini ya Wizara," alisema.

"Nina imani kubwa kwa watumishi wa wizara kuwezesha sekta ya madini kufikia mchango wa asilimia 10 kwenye pato la taifa ifikapo 2025," alisema Mavunde.

Awali, Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa aliwapongeza watumishi wote wa wizara kwa namna wanavyoendelea kujitolea kuhakikisha mikakati yote ya kuendeleza sekta ya madini inafanikiwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Msafiri Mbibo alisema Baraza hilo ni utekelezaji wa wajibu wa mwajiri kwa wafanyakazi na kubainisha kuwa mkutano huo umelenga zaidi kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 na mpango wa bajeti ijayo ya mwaka 2024/2025.

# Hapi ataka viongozi wa CCM kusikiliza kero za wananchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Ally Hapi, amesema hana makundi katika uongozi wake na kuwataka viongozi wa CCM kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi, huku akieleza namna alivyoteuliwa kwa kushtukizwa.

Akizungumza jana baada ya kupokewa makao makuu ya jumuiya hiyo jijini hapa, Hapi alisema; "Rafiki yangu ni yule anayetimiza wajibu wake sina kundi, ubaya wa taasisi hizi ukiingia tu watu wanatengeneza, mimi sina kundi sio muumini wa majungu, makundi mimi ni muumini wa ukweli, haki uhodari katika kazi na matokeo atakayekuwa rafiki yangu ni yule tutakayekutana kwenye haya."

Alisema atasimamia haki, uadilifu na ukweli katika kujenga CCM na jumuiya hiyo.

Aliwataka viongozi ngazi za wilaya na mikoa kuhakikisha kuwa jumuiya inakuwa bora na mfano katika jumuiya zote za chama na ivutie vijana kujiunga kwa wingi. Alisisitiza kuwa CCM ina ilani ambayo ni mkataba kwa wananchi hivyo kuwataka viongozi kuwasikiliza, kuzisemea kero za wananchi ili zipatiwe ufumbuzi.

Hapi alisema akiwa jijini Dar es salaam kwenye mapumziko baada ya shughuli za shamba alipokea simu ikimkataka kufika Ikulu ndani ya dakika 30.

"Sasa kutoka nyumbani kwangu Mbweni hadi Ikulu ni mwendo, nilijitahidi kutumia uzoefu wangu wa serikalini kupita barabarani nikiendesha gari mwenyewe na nilifika ndani ya dakika 35, lakini wakati huo sielewi maana niliambiwa unaitwa nikapokewa nikaingizwa ndani nikawa kwenye gari nikaambiwa subiri humu ndani usihofu."

"Mtu mmoja akaninong'oneza unaona ile gari wapo wenzio, kina nani sijui, wale bwana wakaondoka wakaenda ndani nikaambiwa shuka nikakutana na Makala, Mongela, baadaye Katibu Mkuu (John Nchimbi) akatuchukua tukamuuliza kuna jambo gani? Akasema tumfuate tunaingia mle tunakutana na kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) chini ya uenyekiti wa Rais Samia Suluhu Hassan."

"Mwenyekiti akasema sasa ataanza mwenye umri mdogo nenda pale ukazungumze, sasa nitasema nini? Akasema we nenda nilipofika eneo la kuzungumza akasema NEC imekuthibitisha uwe Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, haya sema ilikuwa tabu kweli. Nina kila sababu ya kushukuru vikao vyote kwa imani kubwa kwangu," alisema.

Alisema jamii ina mmomonyoko wa maadili huku matendo ya ukatili kwa watoto yalishamiri na kuwataka viongozi wa jumuiya hiyo kutambua kuwa wana nafasi ya kusimamia suala hilo.

"Nafasi yetu kama wazazi nchini ni kusimamia ulinzi wa watoto dhidi ya ukatili, na kufuatilia malezi ya watoto kuanzia shule kwakuwa ndio taifa la leo na kesho," alisema.

Aliwataka wazazi kuhakikisha wanakagua suala la mmomonyoko wa maadili na kudhibiti watu wachache wanaotaka kuharibu maisha ya watoto na vijana.

Alisema katika kipindi cha uongozi wake ndani ya jumuiya atahakikisha kuwa mifumo ya Tehama inatumika kukusanya mapato badala ya utaratibu uliopo kwa sasa.

Aidha, alisema atapokea taarifa za mali za jumuiya, changamoto zilizopo, na taarifa kuhusu uhai wa jumuiya kila mkoa huku akiwaagiza wahusika kuandaa taarifa hizo.

Naye, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Mkoa wa Dodoma, Samweli Malecela alisema vijana kuhakikisha wanajenga utamaduni wa kulea wazazi wanapozeeka.

Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo Zanzibar, Ali Issa Ali aliwataka wanaCCM kuhakikisha wanalinda yaliyofanywa na viongozi ili uchaguzi uwe rahisi kwao.



Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana (kushoto). akikabidhi baadhi ya nyaraka kama vitendeakazi kwa Naibu Waziri wa wizara hiyo, Jumanne Sagini wakati wa mapokezi yake, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Makandarasi wazawa washirikishwe utekelezaji miradi'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi Innocent Bashungwa, amesema Makandarasi wazawa wanapaswa kushirikishwa kwa asilimia 100 kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini ili kuiingizia mapato nchi badala ya fedha nyingi kwenda nje ya nchi.

Bashungwa, alisema hayo juzi jijini hapa, wakati wa hafla ya kupongeza serikali ya awamu ya sita katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema, katika uchambuzi wa mwaka 2013 hadi 2023, umebaini ushiriki mdogo wa Makandarasi wazawa katika miradi mbalimbali ya ujenzi.

Alisema, kati ya jumla ya miradi 36,839 yenye thamani ya Sh. trilioni 61.64 iliyosajiliwa na kutekelezwa katika kipindi hicho, wazawa walitekeleza 35,351 yenye thamani ya Sh. trilioni 23.75, sawa na asilimia 38.5 ya jumla ya thamani ya miradi yote.

Alisema ni dhahiri kuwa ingawa wazawa wametekeleza miradi mingi kwa idadi miradi hiyo ina thamani ndogo kuliko michache iliyotekelezwa na wageni.

Alisema wastani wa thamani ya miradi iliyotekelezwa na wazawa ni Sh. milioni 672, wakati wastani wa thamani ya miradi iliyotekelezwa na wageni ni Sh. bilioni 25.5.

"Hii inaonesha kuwa asilimia kubwa ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inawanufaisha wageni kutoka nje ya nchi kuliko wazawa," alisema.

Aidha, alisema serikali imekamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami wenye jumla ya kilometa 1, 198.50 katika kipindi cha miaka mitatu cha Rais Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani mwezi Machi, 2021.

"Katika kipindi cha miaka hii mitatu barabara 25 zimekamilika na 57 zenye urefu wa kilometa 3,794.11 zinaendelea na zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji," alisema Bashungwa.

Aidha, alisema Wizara ya Ujenzi imetenga miradi itakayotekelezwa na wazawa kwa lengo la kuwajengea uwezo makandarasi na wahandisi washauri elekezi wa ndani.

"Katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara inatekeleza miradi 12 ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ambayo imetengwa mahsusi kwa ajili ya Makandarasi Wazawa ikiwemo barabara ya Monduli - Engaruka - Ngareshi - Enguiki (km 11); Kamsamba - Mlowo (km 147); Changombe - Patamela - Mkongolosi (km 30) na Puge - Ziba (km 11)", alifafanua Bashungwa.

Bashungwa alisema katika kipindi cha miaka mitatu sekta ya ujenzi imefanikisha ujenzi wa madaraja makubwa nane yakiwemo Daraja la Wami mkoani Pwani, Daraja la Tanzanite mkoani Dar es Salaam, Daraja la Gerezani mkoani Dar es Salam, Daraja la Mpwapwa mkoani Dodoma, Daraja la Kiegeya mkoani Morogoro, Daraja la Ruhuhu mkoani Ruvuma, Daraja la Kitengule mkoani Kagera na Daraja la Msingi mkoani Singida.

Vilevile, alisema kuwa madaraja matano yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji likiwamo la J.P Magufuli (Kigongo -Busisi) mkoani Mwanza ambao umefikia aslimia 85 Daraja la Pangani, mkoani Tanga umefikia asilimia 23, Daraja la Mbambe mkoani Pwani umefikia asilimia 15 na Daraja la Mpiji Chini mkoani Dar es Salaam.





# Ukiuza viuatilifu kinyemela faini mil.100/- itakuhusu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Afya ya Mimea na Udhibiti wa Viuatilifu Tanzania (TPHPA) imewatangazia kiama wafanyabiashara watakaobainika kuuza viuatilifu bila kupata mafunzo, kwamba itawachukulia hatua kali za kisheria ikiwemo kuwatoza faini ya Sh. milioni 100.

Mkurugenzi wa Usalama wa Afya ya Mimea kutoka TPHPA, Dk. Ben Ngowi alitoa tahadhari hiyo alipomwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo wakati wa kufungua mafunzo ya wauzaji wa viuatilifu kutoka mikoa 12 yaliyofanyika jijini Mbeya.

Alisema biashara ya viuatilifu inasimamiwa na Sheria Namba 4 ya Afya ya Mimea ya Mwaka 2020 ambayo inamtaka kila mfanyabiashara anayeuza viuatilifu awe na mafunzo maalumu ambayo yanatolewa na mamlaka hiyo.

Alisema kwa mujibu wa sheria hiyo, mtu binafsi akikutwa anauza viuatilifu hivyo bila kupata mafunzo anatozwa faini ya kati ya Sh. 50,000 na Sh. milioni 10 ama kifungo cha miaka isiyopungua mitatu gerezani.

Alisema kwa kampuni faini yake ni kati ya Sh. milioni 10 mpaka Sh. milioni 100 na kwamba adhabu hizo zinaenda sambamba na mhusika kufungiwa biashara yake.

"Mafunzo haya huwa yanalenga kuwajengea uwezo wafanyabiashara ili wajue matumizi sahihi ya viuatilifu wanavyoviuza na tahadhari za kuchukua wakati wa kuvitumia ili wawafundishe wakulima sasa mtu asipopata mafunzo haya anaweza akawapotosha wakulima na ndiyomaana sheria imeweka hizi adhabu," alisema Dk. Ngowi.

Alisema wamekuwa wakifanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka yanayouza viuatilifu ili kubaini kama wauzaji wanaelewa taratibu zinazotakiwa kufuatwa.

Mratibu wa mafunzo hayo, Jumanne Msalama aliwataka wakulima kuchunguza viuatilifu wanavyonunua madukani kabla ya kwenda kuvitumia, ili kuepuka kununua viuatilifu feki ama ambavyo muda wake wa matumizi umekwisha.

Alisema viuatilifu vyote ambavyo vimesajiliwa kutumika nchini vina vibandiko ambavyo vimeandikwa maelezo ya namna ya kukitumia kiuatilifu husika na kwamba lazima yawe yameandikwa kwa lugha mbili ambazo ni Kiswahili na Kiingereza.

Alisema kiuatilifu chochote ambacho kinatumika nchini ni lazima kiwe kimesajiliwa na TPHPA na kwamba endapo mkulima ama mfanyabiashara ananunua kiuatilifu husika akibaini kuwa hakina nembo ya mamlaka hiyo anatakiwa kuachana nacho ama kutoa taarifa.

"Kwahiyo tunatoa tahadhari kwa wakulima kuhakikisha wanaponunua viuatilifu wanahakiki ili kubaini kama ni halali ama feki, ukitumia viuatilifu feki vinaweza vikakuletea madhara mwenyewe ama kwenye mazao yako.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Uchumi na Uzalishaji, Dk. Samora Mshang'a aliwataka wafanyabiashara wote wa viuatilifu kuhakikisha wanapata mafunzo ili kukidhi matakwa ya sheria za nchi.

Pia aliwataka wauzaji wote wa pembejeo kuhakikisha wanasajiliwa, wanapata mafunzo na kuwa na vyeti vinavyoonyesha kuwa wamepata mafunzo ili kuepuka kukumbana na mkono wa sheria.

Baadhi ya wauzaji wa viuatilifu walioshiriki mafunzo hayo, waliwaomba maofisa wa TPHPA kutoa mafunzo kwenye mikoa yote nchini ili kuwasaidia wakulima na kulinda afya ya mimea.

Wauzaji wa viuatilifu 145 kutoka kwenye mikoa 12 ikiwemo ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walishiriki mafunzo hayo ambayo huwa yanatolewa kila mwaka.



Wachuuzi wakiwashawishi abiria kununua bidhaa zao, katika eneo la Uyole, jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## CHADEMA: Tuache migogoro, inafifisha nguvu kuikabili CCM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, kimewataka wanachama wake kuepuka migogoro ya wenyewe kwa wenyewe kwa maelezo kuwa inafifisha nguvu ya kukikabili Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwenyekiti wa kanda hiyo, Peter Msigwa alitoa kauli hiyo juzi kwenye mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa chama hicho katika Jimbo la Mbeya Mjini ambapo.

Alisema adui wa chama hicho ni CCM na siyo wenyewe kwa wenyewe.

Msigwa alisema baadhi ya wanachama wa chama hicho wamekuwa wakitumia nguvu kubwa kusigana kwenye mitandao ya kijamii badala ya kutumia nguvu hiyo kupanga mikakati ya kukiondoa CCM madarakani.

Alisema kwenye uchaguzi wa ndani ya chama migogoro huwa lazima itokee lakini inatakiwa kumalizika baada ya uchaguzi kukamilika badala ya kuendeleza.

"Mwaka huu tuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mwakani tuna uchaguzi mkuu, kwahiyo nawaomba uchaguzi huu usitugawe badala yake utuimarishe kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani," alisema Msigwa.

Alisema viongozi wa kanda wamekuwa wakifanya kazi ya ziada kuhakikisha migogoro inayoibuka inamalizwa mapema ili isilete madhara pamoja na toa elimu kwa wananchama.

Hivyo, aliwataka viongozi watakaochaguliwa kuhakikisha wanawaunganisha wanachama wote na kuanza harakati za kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Vilevile alisisitiza wanachama wa chama hicho kuendelea kusajiliwa kidijitali ili kuboresha taarifa za wanachama wa chama hicho na kuwa na uhakika wa kushinda kwenye uchaguzi.

# Mradi upanuzi Barabara Tanzania- Zambia waingia dosari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MRADI wa upanuzi wa Barabara ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kuwa ya njia nne katikati ya Jiji la Mbeya, umeanza kuingia dosari baada ya baadhi ya wananchi kuibuka na madai ya kutolipwa fidia kwa zaidi ya miaka nane licha ya nyumba zao kubomolewa.

Madai hayo yameibuliwa na wananchi zaidi ya 65 wa Kata za Simike na Nzovwe jijini Mbeya ambao walizuiliwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuendeleza makazi yao kwa makubaliano ya kulipwa fidia ili wapishe mradi huo.

Wananchi hao wanadai kuwa wamekamilisha masharti yote ikiwemo kubomoa baadhi ya nyumba zao kwa mujibu wa makubaliano, lakini wamepelekewa maelezo kuwa baadhi yao hawatalipwa kwa sababu ambazo hazieleweki.

Mmoja wa wananchi hao, Emmanuel Mwakalinga alisema walizuiwa kuendeleza makazi yao mwaka 2016 na wakaridhia kwa sababu walikuwa na matumaini ya kulipwa na kwamba hata wao wanapenda maendeleo ndiomaana walikubali.

Alisema hivi karibuni kilifanyika kikao na maofisa wa TANROADS ambao waliwaambia kwamba kuna baadhi yao watalipwa na wengine hawatalipwa jambo ambalo liliwatia wasiwasi kwamba kuna ubabaishaji.

"Sisi wote hapa ni waathirika sasa tunajiuliza kwamba kwa nini wengine walipwe na wengine wasilipwe?, sasa uamuzi wetu ambao tumekubaliana ni kwamba hata wale ambao wapo kwenye orodha ya kulipwa wote tunayakataa malipo hayo mpaka tujuwe hatima ya wenzetu," alisema Mwakalinga.

Naye Akley Matoi ambaye ni mkazi wa Meta, alisema wananchi wote walikuwa washirikiana kwenye kila hatua na walikuwa wanafanya vikao na serikali ili kujua hatima yao lakini kwa sasa wameanza kutenganishwa.

Alisema waliambiwa wabomoe nyumba zao kwa hiyari baada ya kuhakikishiwa kwamba watalipwa na wakatekeleza jambo ambalo limekuwa kinyume hatua za mwisho.

Alisema kwa sasa wameambiwa kwamba kuna baadhi ya nyumba ambazo tayari zimebomolewa hazitapitiwa na barabara hiyo na hivyo waliobomoa nyumba hizo hawatalipwa.

"Tulitakiwa tuanze kulipwa fidia zetu tangu Aprili 1 mwaka huu lakini sasa wamekuja na maelezo ambayo yanatukatisha tamaa, tunaomba serikali itusaidie maana tumegeukwa katika hatua za mwisho," alisema Matoi.

Rhoda Mwaitebela alisema wanayo mikataba ambayo waliisaini kwa ajili ya kulipwa fidia na serikali na hivyo taarifa ya kwamba hawatakiwi kulipwa imeanza kuwasababishia maumivu ambayo walikuwa hawayatarajii.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mbeya, Masige Matari alikiri kuwepo kwa malalamiko ya wananchi na kwamba kilichosababisha ni baadhi yao kupatiwa fomu na mikataba kimakosa wakati wa uthaminishaji wa awali.

Alisema walipopitia upya ramani ya barabara hiyo walibaini kuwa kuna baadhi ya nyumba ambazo ziliingizwa kwenye mradi huo lakini kwenye utekelezaji hazitaguswa kabisa na kwamba ndiomaana waliamua kusitisha.

Alisisitiza kuwa serikali haiwezi kuwalipa watu ambao mradi hautawagusa kabisa.

# Ongezeko la taka Zanzibar lamshtua Makamu wa Rais

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka mamlaka zinazohusika na usimamizi wa mji Zanzibar kuhakikisha wanaongeza nguvu maalum katika kuweka usafi zaidi kwa sababu kiwango cha uzalishaji taka mjini kimeongezeka.

Aliyasema hayo juzi baada ya kufanya ziara maalumu ya kukagua na kuangalia shughuli za biashara kwa maandalizi ya Sikukuu ya Eid-El- Fitri visiwani Zanzibar katika mitaa ya maduka ya Mlandege, Mchangani na Darajani Unguja.

Allisema katika kipindi cha kuelekea Sikukuu ya Eid- El-Fitri shughuli na harakati za kibiashara huongezeka mara dufu kwa watu wanaotafuta mahitaji mbalimbali, jambo ambalo linakwenda sambamba na ongezeko la uzalishaji wa taka katika maduka mbali mbali yaliyopo kwenye mitaa hiyo.

Alisema hali hiuo huleta changamoto ya uchafu katika mji jambo ambalo linahitaji mkakati na juhudi maalum katika kuhakikisha kwamba mji wote unakuwa na mazingira safi wakati wote.

Alisema kwamba ni lazima mamlaka zinazohusika na usafi kuhakikisha wanakuwa na mkakati sahihi wa kupambana na hali hiyo kwa kuwepo utaratibu maalum wa kufanya usafi.

Kuhusu madai ya uwapo ongezeko la watu wanaoishi nchini isivyo halali, alisema serikali italifanyia kazi suala hilo hasa kwa vile Zanzibar haikatai wageni bali inahitaji watu waishi kwa ustaratabu na nidhamu.

Awali baadhi ya wafanyabiashara walimueleza Makamu wa Rais kwamba ipo changamoto kubwa ya wimbi la wageni ambao wanadaiwa kuishi katika mazingira yya kutishia usalama.

# Serikali kufanya mageuzi sekta ya anga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhammed amesema Serikali ya Zanzibar imedhamiria kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya anga visiwani hapa yenye lengo la kuimarisha miundombinu na utoaji wa huduma katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, kuhusu maendeleo ya sekta ya anga.

Waziri huyo alisema kutokana na uimarishaji wa miundombinu na utoaji wa huduma katika uwanja huo umeingia katika ramani ya kuwa kiwanja bora barani Afrika na dunia ambapo dhamira hiyo ilianza kwa vitendo mnamo mwaka 2021.

Alisema serikali iliona haja ya kuzikaribisha kampuni zenye uwezo wa utoaji wa huduma bora duniani ili kusaidiana na wazawa kuleta mabadiliko chanya Zanzibar ambayo yatasababisha kukuza sekta ya kiuchumi ikiwemo ya utalii na biashara.

Akieleza baadhi ya mafanikio yaliopatikana ndani ya muda mfupi baada ya Serikali ya Awamu ya Nane kuingia madarakani ikiwemo kuongezeka kwa abiria wanaoingia na kutoka Zanzibar kwa kutumia viwanja vya ndege kutoka abiria 1,609,235 mwaka 2019 hadi abiria 1,940,548.

Alisema kupitia Kampuni ya Dnata April mwaka 2023 Uwanja wa Ndege Karume ulipata cheti cha utoaji wa huduma za usafirishaji wa mizigo na kuwa wakala aliyethibitishwa na Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga wa Umoja wa Nchi za Ulaya ambao ni mpango salama wa usafirishaji na usambazaji ulioazishwa na Umoja wa Ulaya (EU).

"Na hivyo kwa sasa hakuna changamoto yoyote ya kiusalama ya wananchi wa Zanzibar wanaokusudia kusafirisha mzigo na bidhaa zao barani ulaya," alisema.

Aidha, alisema kupitia kampuni ya Emirate leisure retail, Uwanja wa Ndege wa Karume ulipata tunzo ya kiwanja bora kilichofanya mabadiliko makubwa katika huduma ya vyakula na vinjwaji.

Alisema uwanja huo pia umepata alama A kwenye ukaguzi wa ulinzi na usalama wa viwanja vya ndege duniani, uliofanywa na wakaguzi kutoka shirika lenye dhamana ya usimamizi wa usafiri wa anga duniani na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nafasi ya nne Afrika.

Alisema serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri wa anga Zanzibari ikiwemo ujenzi, ukarabati na maboresho ya jengo la kwanza na la pili la abiria la AAKIA.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud (wa pili kulia), akiangalia viatu, alipofanya ziara katika maduka mbalimbali Mjini Unguja jana, kwa ajili ya kuangalia mwenendo wa biashara kwa kipindi hiki cha kuelekea Sikukuu ya Eid el fitri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bei ya mafuta Zanzibar Aprili yapanda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imetangaza bei mpya za mafuta, ambapo mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya ndege yameendelea kupanda kwa mwezi huu.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari katika ofisi ya mamlaka hiyo, Meneja Kitengo cha Uhusiano wa mamlaka hiyo, Mbaraka Hassan Haji, alisema bei ya mafuta ya petroli mwezi huu itakuwa ni Sh. 3,133 kutoka Sh. 3,118 ya mwezi uliopita.

Alisema ongezeko hilo ni tofauti ya Sh. 16 kwa lita ikiwa ni tofauti ya asilimia 0.51.

Aidha alisema kwa mafuta ya dizeli mwezi huu yatauzwa kwa Sh. 3,165 kutoka Sh. 3,114 ya mwezi uliopita ambapo ni tofauti ya Sh. 51 kwa lita ikiwa ni tofauti ya asilimia 1.64. Mbaraka alisema kuwa mafuta ya ndege kwa mwezi huu yatauzwa kwa Sh.2,792 kutoka Sh. 2,764 kutoka Sh. 2,636 ya mwezi uliopita, tofauti ya Sh. 128 kwa lita na tofauti ya asilimia 27, akisema mafuta ya taa yataendelea kuuzwa kwa bei ile ile ya Sh. 3,200.

Akizungumzia sababu za kuongezeka kwa bei za mafuta kwa mwezi huu alisema ni kuongezeka kwa gharama za mafuta katika soko la dunia, gharama za uingizaji wa mafuta pamoja na mabadiliko ya fedha za kigeni.

Alisema kuwa ZURA inapanga bei kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwemo wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani, gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es salam na Tanga na gharama za mabadiliko ya fedha za kigeni zinazotumika kununulia mafuta

Sababu zingine ni gharama za usafiri, bima na premium hadi Zanzibar, kodi na tozo za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Alisema pamoja na kupanda kwa bei hizo lakini Zanzibar ina rasilimali hiyo ya kutosha katika bohari zake zilizokuwepo Maruhubi na haitegemei kupata upungufu wa mafuta.

"Zanzibar tuna vituo vya mafuta zaidi ya 100, hivyo hakuna athari yoyote itakayojitokeza katika suala la upungufu wa bidhaa hii ya mafuta," alibainisha.

Hivyo, alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi kununua mafuta katika vituo halali na kudai risiti za kielektroniki kila wanapofanya manunuzi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi akijumuika na viongozi na wananchi katika maziko ya mwili ya Burhan Saadat Haji, aliyewahi kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni na Waziri wa SMZ, kijijini kwao Kiembesamaki, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Kanuni mpya ununuzi wa umma mbioni kukamilika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Fedha kwa kushirikiana na taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma, ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), inaendelea kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024.

Lengo la kuandaa kanuni hizo mpya ni kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023, imebainishwa.

Pia imeelezwa kuwa zaidi ya Sh. trilioni 29 zimewekwa kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) kwa ajili ya kufanya ununuzi wa bidhaa, huduma na kazi za ujenzi na kwamba kufikia jana, mikataba yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 5.14 imetolewa kwa wazabuni.

Akizungumza jana kuhusu mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa PPRA, Mkurugenzi wa Huduma za Ushauri na Kujenga Uwezo wa mamlaka hiyo, Amini Mcharo, alisema sheria hiyo imeweka mazingira rafiki zaidi yanayolenga upatikanaji wa thamani halisi ya fedha katika utekelezaji wa ununuzi wa umma, ikiwamo kupunguza muda wa mchakato wa zabuni.

Mcharo alisema mambo yaliyozingatiwa ni kuondoa sharti la nyongeza ya adhabu kwa kampuni zilizofungiwa nje ya nchi; kuweka mazigira rafiki zaidi kwa makundi maalumu, vijana, wanawake na wazee katika kushiriki kwenye zabuni za umma; kuongeza fursa za upendeleo kwa watu na kampuni za ndani; kufungamanisha mnyororo mzima wa ununuzi na ugavi; matumizi ya bei kikomo kwa bidhaa na huduma zenye bei kikomo.

"Lengo pia ni kupunguza mlolongo wa uidhinishaji katika michakato ya zabuni; uandaaji na uwasilishaji wa taarifa ya tathimini ya ununuzi wa umma kwa Rais; kuweka sharti la lazima kuchakata zabuni za umma kupitia mfumo wa ununuzi kielektroniki. Lengo ni kuongeza uwazi, ufanisi na kupunguza uwezekano wa rushwa katika zabuni za umma. Zaidi, Sheria imeweka ukomo wa utekelezaji miradi ya kazi za ujenzi kwa matumizi ya rasilimali za ndani," alisema.

Kuhusu mfumo wa NeST, Mcharo alisema wazabuni 18,101 wamejisajili na kwamba mfumo umeunganishwa na mifumo 17 ya serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi, kupunguza muda na gharama za michakato ya ununuzi, kudhibiti vitendo vya udanganyifu, rushwa na kuzuia ukosefu wa maadili.

Pia alisema kutokana na ushiriki wa makundi maalum katika ununuzi wa umma hadi Februari, mwaka huu, tuzo za mikataba zenye thamani ya Sh. bilioni 1.95 zimetolewa kwa makundi hayo kupitia zabuni za umma zilizotangazwa na taasisi za ununuzi kupitia mfumo huo.

Alisema kundi la vijana limepata tuzo za mikataba zenye thamani ya Sh. milioni 709, wanawake Sh. bilioni 1.2 na wazee Sh. milioni 78.3.

# Serikali yatia saini mradi bilioni 96/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetia saini makubaliano na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) mkataba wa msaada wa Euro milioni 34.86 sawa na Sh. bilioni 96.47 kwa ajili ya mradi wa kufua umeme wa nguvu za maji wa Kakono mkoani Kagera.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, alisema hayo jana jijini Dodoma wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba huo baina ya wizara na AFD.

"Kama mnavyofahamu, mtambo unaotarajiwa kujengwa wa kufua umeme wa Kakono uko Mto Kagera, takriban kilometa 90 magharibi mwa Manispaa ya Bukoba, ni kona ya kaskazini magharibi mwa Tanzania"alisema

Alisema lengo la mradi ni kuongeza uzalishaji wa umeme nafuu wa nguvu za maji ili kukabiliana na upungufu wa umeme katika gridi ya taifa maeneo ya Kaskazini Magharibi mwa Tanzania.

Alisema ujenzi wa mtambo wa Kakono, utakuwa mbadala wa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia mafuta ambayo hutumika kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa umeme kwenye gridi ya taifa ili kupunguza mgawo.

"Utekelezaji wa mradi huu unaendelea na utakamilika mwaka 2026 na kukabidhiwa kwa serikali rasmi Desemba, 2028. Mradi unatarajiwa kuongeza megawatt 87.8 kwenye gridi ya taifa utakapokamilika," alisema

Pia alisema mradi huo unafadhiliwa kwa pamoja na wafadhili watatu ambao ni ADF (Euro milioni 110 sawa na Sh. bilioni 304.37), Benki ya Maendeleo ya Afrika (dola za Marekani milioni 161.47 sawa na Sh. bilioni 413.95) na Umoja wa Ulaya (Euro milioni 34.86 sawa na Sh. bilioni 96.47).

"Leo tumetia saini huu mkataba wa mwisho ambao ulikuwa haujatiwa sainiwa wenye msaada kutoka Umoja wa Ulaya, utakaosimamiwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa kama nilivyosema.

"Kwa ujumla, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wafadhili hawa watatu niliowataja kwa michango yao kwa ajili ya mradi huu muhimu" alisema

Alisema mradi wa kufua umeme wa Kakono, unaendana na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao una maudhui ya kujenga uchumi shindani na wa viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu kupitia uboreshaji wa miundombinu, upatikanaji wa nishati ya uhakika, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na mifumo ya elimu na ujuzi.

Pia alisema mradi huo unaendana na mkakati wa Benki ya Maendeleo ya Afrika wa mwaka 2021 hadi 2025 kwa Tanzania na vipaumbele vya kiuendeshaji vinavyojulikana kama "High Fives" vya Benki hiyo, ambapo katika vipaumbele hivyo, sekta ya nishati ni namba moja.

Mkurugenzi Mkazi wa AFD, Celine Robert, alisema wamekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na Tanzania hivyo wataendelea kusaidia katika sekta ya nishati kifedha na kiufundi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, alisema wanaishukuru AFD kwa msaada huo na wanaahidi mradi huo kukamilika kwa wakati na kwa ubora.


## KUPOTEA KWA CHETI



**UPENDO JOHN MWAMPAGAMA**

Anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo cha stashahada ya elimu ya msingi kilichotolewa na chuo cha St.Agrey Teacher's College Mbeya,namba ya cheti ni **0092513,** pia namba ya usajili ni **NS0211/0078/2002.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBE/7935/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BONIPHACE JOHN MNYOGORO**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 321 AAQ Toyota Hiace . ENGINE NO **3Y0688844,** CHASSIS **NO YH71B7003027** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi . TAARIFA YA POLISI: **PHQ/KIL/MOS/ 6788/2024**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 14/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU EUGEN NKOKO MAGANGA wa MIYUJI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ELIAS EUGEN NKOKO**

**TANGAZO**

**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 04 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 04 Mwezi 04 Mwaka 2024.

..........HAKIMU

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**RUFAA YA MADAI NA 10/2023**

**(Kutoka shauri la Marejeo Na 1/2023 kutoka Mahakama ya Wilaya Songwe,asilia shauri la maombi ya madai na 21/2021 ya Mahakama ya Mwanzo Mwambani mbele ya Mh.E.E.Mtengeti)**
**ZAKAYO MATIGA..................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**SAID MOHAMED SOOD, FAGIO COURT BROKER, GASTORY MARANDU.....WAJIBU RUFAA**

**KWA BWANA: FAGIO COURT BROKER**

**POPOTE ULIPO-TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI**

Unaamuliwa na Mahakama hii,kuhudhuri hapa Mahakamani siku ya tarehe 09/05/2024 siku ya Jumanne saa 3:00 asubuhi bila kukosa. ELEWA KWAMBA,ukikosa kufika siku hiyo,shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 04/04/2024.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**


## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**GREVEN GERALD MSENGA**

anatangaza kupotelewa na kadi za bajaji zenye namba za usajili **MC 640 BBD** yenye Chassis namba **MD2AA24ZZTWJ92243 na T 932 BVK** yenye Chassis namba **MD2AAAAZZUWA12934.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/58594/2024.**


**IN THE DISTRICT COURT OF KIBAHA**
**AT KIBAHA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5970 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FABIAN MUNGERERE MAJAGA OF KIBAHA**

**AND**

**In the matter of Application for Letters of Administration of the Estate**
**JOSEPHINE NYAKUBIA MUNGERER BEKER (nee MUNGERERE.....PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 30th day of April, 2024.
Dated at Kibaha this 4th day of April, 2024.

Senior Resident Magistrate

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

HABARI KIMATAIFA

## Israel yapanga kuivamia tena Rafah

**JERUSALEM,** ISRAEL

WAZIRI Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu amesema tayari wameshapanga tarehe ya kuuvamia mji wa Rafah licha ya kutotaja siku husika watakayotekeleza hilo, ikiwa ni saa 24 baada ya jeshi la nchi hiyo kusema limepunguza wanajeshi wake waliokuwa kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Baada ya kiongozi huyo kutoa kauli hiyo jana, Marekani ilikosoa vikali tangazo hilo ikisisitiza kwamba operesheni ya kijeshi kwenye mji huo itakuwa na athari kubwa hasa kwa watu waliojihifadhi kwenye eneo hilo, baada ya kukimbia mapigano katika Ukanda wa Gaza.

"Leo nimepokea ripoti ya kina juu ya mazungumzo ya Cairo na tunayafanyia kazi mara kwa mara ili kufikia malengo yetu, kwanza kabisa kuachiliwa mateka watu wote na kupata ushindi kamili dhidi ya Hamas. Ili kupata ushindi huu tunalazimika kuingia ndani ya Rafah na kuvimaliza vikosi vya kigaidi vilivyoko huko. Tutafanya hivyo. Tayari tarehe imepangwa," alisema Netanyahu.

Ilielezwa kuwa mipango ya Israel ya kuivamia Rafah kijeshi imekuwa ikipingwa vikali na washirika wake wa kimataifa kutokana na kuongezeka kwa mzozo wa kibinadamu katika Ukanda wa Gaza.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Marekani, Matthew Miller, alisema hawajabadilisha msimamo wao wa kupinga mpango wa Israel wa kuivamia kikamilifu Rafah.

Tangu mwezi Februari, Marekani ilionya juu ya uvamizi huo ikisema utaibua mzozo mkubwa wa kibinadamu kwa kuwa zaidi ya Wapalestina milioni moja wamejihifadhi kwenye mji huo wakiyakimbia mapigano yanayoendelea katika maeneo mengine ya Gaza.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya inayoratibiwa na Hamas katika Ukanda wa Gaza, idadi ya Wapestina waliokufa hadi sasa kutokana na mapigano imependukia 33,200 na karibu 76,000 walijeruhiwa tangu vita hivyo vilipoanza Oktoba 7 mwaka 2023.

Aidha, huko Cairo, taarifa zinasema wapatanishi kwenye mzozo huo wamewasilisha pendekezo la makubaliano mapya ya kusitisha mapigano kwa wawakilishi wa Hamas na Israel.

Ilielezwa kuwa makubaliano hayo, yatakayotekelezwa kwa wiki sita, yatajumuisha usitishwaji wa mapigano na makubaliano ya Hamas kuwaachia mateka 40 wa Israel na Israel kuwaachia wafungwa karibu 700 wa Kipalestina wanaozuiwa nchini humo.

**DW**

# Wanasheria wataka Mahakama kumshitaki Donald Trump

**WASHINGTON,** MAREKANI

TIMU ya mwanasheria maalum wa Marekani, Jack Smith, imetoa pendekezo kwa Mahakama ya Juu kuyakataa madai ya rais wa zamani, Donald Trump, kwamba ana kinga ya kutoshitakiwa kwenye kesi ya njama ya kugeuza matokeo ya uchaguzi wa 2020.

Taarifa ya waendesha mashitaka hao iliwasilishwa usiku wa kuamkia jana kwenye Mahakama ya Washington, ikiwa ni wiki mbili tu kabla ya majaji kuamua endapo rais huyo wa zamani ashitakiwe ama ala kwa kile alichokitenda wakati akiwa kwenye Ikulu ya 'White House'.

Wanasheria hao waliiandikia mahakama kwamba njama ya Trump kutaka kutumia madaraka yake kubadili matokeo ya uchaguzi na kuhujumu makabidhiano ya madaraka yalikuwa mambo yanayokinzana kabisa na vifungu vya katiba vinavyoilinda demokrasia ya Marekani.



Aidha, ilielezwa kuwa uamuzi wa mwisho unatarajiwa tarehe 25 mwezi huu na kwamba ndio utakaotoa muelekeo wa kesi hiyo dhidi ya Trump, ikiwa ni takribani miezi saba kabla ya uchaguzi mkuu, ambao bilionea huyo wa chama cha Republican anatazamiwa kuchuwana tena na Joe Biden wa Democrat.

**OMBI LAPINGWA**

Katika hatua nyingine jaji mmoja wa mahakama ya rufaa ya New York alipinga ombi la Trump, la kuchelewesha kesi yake ya jinai ya Aprili 15, wakati akipambana kuondoa kesi hiyo kutoka mji wa Manhattan, huko New York.

Uamuzi huo ulitolewa juzi, ikiwa ni wiki moja kabla ya uteuzi wa jopo la mahakama kuanza. Ikielezwa kuwa mawakili wa Trump walikuwa wamewasilisha hoja katika kikao cha dharura, wakidai kwamba kesi hiyo ya kihistoria inapaswa kuahirishwa, wakati wakitetea haja ya kuihamisha kutoka mji wa Manhattan wenye wafuasi wengi wa chama cha Democratic.

Trump alipendekeza kupitia jumbe za mitandao ya kijamii kwamba kesi hiyo ihamishiwe Staten Island, jimbo pekee la New York ambalo alishinda katika uchaguzi wa mwaka 2016 na ule wa 2020.

**DW, VOA**



Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa (wakwanza kushoto) akizungumza na mwenzake wa Rwanda, Paul Kagame, kuhusu kuweka sawa hali ya kisiasa DRC. **PICHA: MTANDAO**

# Wanajeshi watatu wa Tanzania wauawa DRC

**KINSHASA,** DRC

WANAJESHI watatu wa Tanzania wanaohudumu katika kikosi cha kutunza amani cha kijeshi cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wameuawa kwenye shambulio la kombora mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na SADC, wanajeshi wengine watatu wanasemekana kujeruhiwa. Licha ya kutotolewa maelezo zaidi kuhusu ni wapi au lini shambulio hilo lilifanyika, au nani aliyelitekeleza.

Aidha, ilibainishwa kuwa Februari, mwaka huu wanajeshi wawili wa Afrika Kusini waliuawa kwenye shambulio kama hilo katika jimbo la Kivu Kaskazini walikokuwa wakilinda amani.

Hata hivyo, katika miezi ya hivi karibuni, maelfu ya watu wamekimbia ghasia zinazoendelea katika maeneo ya mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo licha ya vikosi kutoka mataifa mbalimbali kutumwa katika taifa hilo kuimarisha ulinzi.

Vile vile, ilielezwa kuwa wengi wamejificha katika mji mkuu wa eneo hilo wa Goma, huku wengi wao wakihofia kwamba M23 wanaweza kuuteka, kama walivyofanya mwaka 2012.

Pia ilielezwa kuwa shinikizo limeongezeka kwa serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo baada ya kuamuru tume kubwa ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa (UN) kuondoka nchini humo ifikapo mwisho wa mwaka huu.

Katika hatua nyingine ilibainishwa kuwa Rais wa Rwanda, Paul Kagame alikutana na mwenzake wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa alipowasili nchini humo kwa ajili ya kushiriki kumbukumbu ya miaka 30 ya mauaji ya kimbari, na kuthibitisha uungaji mkono wao katika kutafuta hali ya kisiasa katika mzozo unaoendelea DRC.

"Nadhani tulikuwa na mjadala mzuri sana, ufahamu mzuri sana wa hali hiyo, na labda njia bora zaidi tunaweza kufanya kazi pamoja kutatua hilo, niliridhika," Rais Kagame alisema.

Rais Ramaphosa aliwaambia waandishi wa habari kwamba aliondoka akiwa na nguvu na nia mpya ya kutatua masuala yanayoikumba DRC, ambayo imekumbwa na ghasia kwa zaidi ya miongo mitatu.

Ilielezwa kuwa kutumwa kwa Jeshi la Afrika Kusini nchini DRC kulisababisha mvutano na Rwanda, ambayo inashutumu jeshi la Congo kwa kushirikiana na waasi wanaoitishia nchi yao.

**BBC**

# COASTAL YADAI KUSHTUKIA NJAMA ISICHEZE SHIRIKISHO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imedai kushtukia njama za baadhi ya watu wenye dhamira mbaya ili kuwachanganya wanachama, mashabiki, viongozi, wachezaji na benchi la ufundi ili tu isifanikiwe kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Abbas El Sabri, alisema jana kuwa kwa sasa kuna njama zinatengenezwa makusudi ili Coastal Union isiongee lugha moja, kutokana na kuona ipo kwenye mafanikio makubwa baada ya miaka mingi, ikiwa karibuni kabisa kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho Afrika.

Alisema taarifa kuwa timu hiyo inamjadili kocha David Ouma, na inatarajia kumtimua na kumchukua Goran Copunovic, aliyeonyeshwa mlango wa kutokea na Klabu ya Tabora United, ilitolewa kwa makusudi na wasioitakia mema klabu yao na kwa sasa wapo kwenye uchunguzi wa kujua ni kina nani wanaozusha mambo hayo.

"Hivi nani asiyejua ubora ya David Ouma, ametutoa katika nafasi ya 14 ya Ligi Kuu, sasa tupo kwenye nafasi ya nne na tunakaribia kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao, tutakuwa wendawazimu kiasi gani tuachane na kocha huyu? Tutakuwa wendawazimu kiasi gani kumjadili kocha ambaye anatuwezesha sasa tutembee kwa kujidai na kutamba?

"Hizi ni njama na tumeshawaambia wanachama wetu na mashabiki wetu wazipuuze taarifa hizi kwa sababu zinakuja mahsusi kabisa kwa ajili ya kututoa kwenye reli kuelekea kupambania malengo ya klabu kwa msimu ujao, kwa sasa tuna mechi tatu za nje kwenye Ligi Kuu, tumeshaingia hatua ya robo fainali ya Kombe la FA," alisema.

Coastal Union kwa sasa ipo nafasi ya nne, ikiwa na pointi 30 kwa mechi 21 ilizocheza, na imekuwa timu ya kutisha tangu iwe chini ya Mkenya, Ouma.

Imebakisha mechi tisa, ikiwa na michezo mitatu mfululizo ugenini, Aprili 12 ikitarajiwa kucheza dhidi ya Mashujaa FC, Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma, dhidi ya Namungo, Uwanja wa Ruangwa mkoani Lindi, Aprili 17 na baadaye Yanga, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, mchezo ambao haujapangiwa tarehe.

## Tukuyu Stars, leo tena hoi

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara mwaka 1986, Tukuyu Stars ya Mbeya, wameanza vibaya hatua ya nane bora, Ligi ya Mabingwa Mikoa, baada ya juzi kudunguliwa bao 1-0 dhidi ya Arusha City katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma, kusaka timu tatu zitakazopanda Ligi Daraja la Pili Tanzania Bara.

Bao pekee la washindi katika mechi hiyo ya Kundi B, lilifungwa na Jackson Mbaga dakika ya nane ya mchezo.

Baada ya mechi hiyo ya mapema, baadaye kulikuwa na mchezo mwingine wa kundi hilo kati ya Leo Tena ya Kagera na Housing FC ya Njombe.

Katika mechi hiyo, Housing ilianza vema ligi hiyo kwa kuichapa Leo Tena mabao 2-1.

Housing, ambayo ilitolewa kwenye Raundi ya Pili ya Kombe la FA, ikizabuliwa na Yanga mabao 5-1, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Januari 30, mwaka huu, ilipata mabao yake kupitia kwa Christopher Kidava na Costa Mwihomeke, huku bao la kufutia machozi la Leo Tena likiwekwa wavuni na Ally Mturi James.

Kocha wa Gunners ya Geita ambayo iliifunga Bukombe Combine ya Geita bao 1-0, katika moja kati ya mechi za ufunguzi kwenye Kundi A, Juma Ikaba, amesema ushindi walioupata umewafanya kujiandaa kwa mechi inayofuata dhidi ya Moro Kids bila presha yoyote.

Akizungumza wakati wa mazoezi ya timu yake kwenye maandalizi ya mechi hiyo, Ikaba, ambaye ni kiungo wa zamani wa CDA ya Dodoma iliyotamba kwenye Ligi Kuu (Ligi Daraja la Kwanza enzi hizo) miaka ya 1980, alisema siku zote katika mechi za makundi ushindi ni muhimu katika mchezo wa kwanza, la sivyo timu inajiweka katika wakati mgumu.

"Siku zote mechi za kwanza ni ngumu, ukishinda mechi ya kwanza kama kocha inakuweka vizuri kujiandaa na presha katika mchezo wa pili, ukifungwa mchezo wa kwanza inakuondoa mchezoni kabisa, lakini sisi pointi tatu tulizozipata dhidi ya Bukombe zimeendelea kutuimarisha zaidi na kutupa ujasiri na kujiamini kuelekea kwenye mechi yetu dhidi ya Moro Kids," alisema.




Meneja Mauzo wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Roman Degeleki (kulia), akikabidhi zawadi ya kofia kwa mteja wa benki hiyo tawi la Songea mkoani Ruvuma, Emily Lucas, ambaye ni mkazi wa Paradiso, baada ya kufungua akaunti mpya inayofahamika kama Pesa Akaunti. Makabidhiano hayo yalifanyika wakati wa kuchezesha droo ya kila mwezi ya Pesa Akaunti ambapo wateja watano walijinyakulia zawadi ya Sh. milioni moja kila mmoja. **MPIGAPICHA WETU**

# NMB yawajaza noti washindi wake

**Na Mwandishi Wetu,**
SONGEA

WATEJA watano wa Benki ya NMB wamejinyakulia fedha taslimu Sh. milioni moja kila mmoja katika droo ya kila mwezi iliyochezeshwa katika tawi la NMB Songea kupitia Kampeni ya Pesa Akaunti.

Wateja walioshinda droo hiyo ya mwezi ni Alhami Shemkay, Msimu Mwnyimvua, Abdala Msimu, Emanue Masawe na Unior Mtweve.

Kampeni hiyo inaendeshwa na benki hiyo ikihamasisha Watanzania kutumia Benki ya NMB kuweka fedha, kufungua akaunti na kupata mikopo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo kilimo.

Meneja wa Mauzo wa NMB Kanda ya Kusini, Roman Degeleki, alisema jana kuwa Pesa Akaunti inafunguliwa kwa gharama ndogo kuanzia Sh. 1,000 na haina kianzio cha fedha na mteja hapewi kadi badala yake anaunganishwa moja kwa moja na simu yake ya mkononi.

Alisema akaunti hiyo inamwezesha mteja kufanya matumizi na malipo mbalimbali ikiwamo kulipia Luku, kulipia king'amuzi, kulipa bili za maji na vitu vingine kulingana na mahitaji ya mteja husika.

Kwa mujibu wa meneja huyo, kupitia Pesa Akaunti, mteja anaweza kuchukua mkopo hadi Sh. 500,00 kupitia simu yake ya mkononi bila kuweka dhamana yoyote na kurejesha mkopo huo kwa kutumia simu yake.

Degeleki alitaja faida nyingine ya Pesa Akaunti ni mteja kupata bima ya simu ambayo ikipata changamoto yoyote, benki ina uwezo wa kuifanyia matengenezo simu hiyo bila kujali gharama zake.

Alitoa rai kwa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo kwa kuendelea kufungua akaunti na kuweka fedha kwenye Benki ya NMB ili wanufaike na huduma zinazotolewa katika kila wilaya na mkoa nchini.

Kaimu Meneja wa NMB Tawi la Songea, Mwalimu Mbwambo, alisema droo ya mwezi imehusisha wateja ambao waliweka fedha kwenye akaunti zao kuanzia kiwango cha fedha kisichopungua Sh. 50,000.

Mkaguzi na Mdhibiti wa Michezo ya Kubahatisha kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT), Salim Bugufi, alisema kampeni hiyo inafanyika chini ya uangalizi wa bodi hiyo ili kujiridhisha mtu anayepata fedha hizo kuwa ni mteja halali wa NMB.

Mkazi wa Kijiji cha Ligera, wilayani Namtumbo, Silaji Mango, alipongeza benki hiyo kwa kuendesha droo hiyo ambayo imehamasisha watu wengi kutumia Benki ya NMB kwa kufungua akaunti na kuweka fedha.

## ZISIKUPITE

**SALAH AKOMALIWA SAUDIA**
MOHAMED Salah anatarajiwa kuwaniwa na Klabu za Ligi Kuu Saudi Arabia msimu huu wa majira ya joto huku Al-Ittihad ikijiandaa kutoa pauni milioni 70 kwa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 31 wa Liverpool na Misri. (*Talksport*)

**WILLIMAS ATAKIWA CHELSEA**
Chelsea inajaribu kuwapiku wapinzani wao na kutoa ofa ya pauni milioni 43 kwa mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Nico Williams mwenye umri wa miaka 21, kabla ya dirisha la uhamisho kufunguliwa. (*Football Insider*)

**PAQUETA NA MAN CITY**
KLABU ya Manchester City imekubaliana na kiungo wa West Ham, Lucas Paqueta, kabla ya uhamisho wa majira ya joto. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, alihusishwa kuhamia Etihad mwaka jana. (*Foot Mercato*)

**ONANA AWINDWA ARSENAL**
EVERTON pia inaweza kutarajia ofa kwa kiungo wa Ubelgiji, Amadou Onana huku Ofisa Mtendaji Mkuu wake wa zamani, Keith Wyness, akisema klabu hiyo inaweza kupata hadi pauni milioni 70 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, Arsenal, Newcastle United na West Ham zinamuwania. (*Football Insider*)

**PSG YAKOMAA NA GAVI**
KLABU ya Paris St-Germain haijakata tamaa katika kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona na Hispania, Gavi mwenye umri wa miaka 19, msimu huu wa majira ya joto licha ya kifungu cha kutolewa kwa mchezaji huyo kuwa ni euro bilioni moja. (*L'Equipe*)

**AMORIM MIAKA MITATU**
LIVERPOOL imempa Kocha wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, mkataba wa miaka mitatu kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp huko Anfield. (*Pedro Sepulveda*)

**ADARABIOYO AGOMBEWA**
KLABU ya West Ham imeungana na Liverpool, Tottenham Hotspur na AC Milan katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa kati wa Fulham, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye mkataba wake unamalizika msimu wa majira ya joto. (*Guardian*)

**BRUNO, RASHFORD WATAJWA**
CHELSEA inapaswa kuwavutia kiungo wa kati wa Ureno, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 29 na mshambuliaji wa England, Marcus Rashford (26), kutoka Manchester United msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa mlinzi wa zamani wa Blues, William Gallas. (*Mirror*)

**BENTO AWANIWA INTEr**
CHELSEA haina nia ya kumsajili mlinda lango wa Athletico, Paranaense Bento mwenye umri wa miaka 24, lakini Inter Milan wanatazamiwa kukabiliwa na ushindani kutoka kwingineko kwenye Ligi Kuu England kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil. (*Gazetto dello Sport*)

**BAKAYOKO ATAKIWA DORTMUND**
KLABU ya Borussia Dortmund ina nia ya kumsajili winga wa PSV Eindhoven, Johan Bakayoko mwenye umri wa miaka 20. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ubelgiji pia anaripotiwa kulengwa na Burnley na Brentford. (*Voetbal International*)

**BRANTHWAITE HAJAAMUA**
MLINZI wa Everton na England, Jarrad Branthwaite, amesema anazuia kelele kuhusu mustakabali wake huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, akiivutia Manchester United na Real Madrid. (*90min*)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# CASEMIRO: MAN UTD INANIKOSESHA USINGIZI

**MANCHESTER,** England

CASEMIRO amekiri kwamba kiwango cha Manchester United msimu huu kimemsababishia kukosa usingizi usiku na kuongeza kuwa klabu hiyo inahitaji kuwa na mawazo ya "siku hadi siku" na kutoathirika na na mbio za kuwania taji au nafasi za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**United ipo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu England ikiwa na pointi 49, nyuma ya pointi 11 dhi di ya Tottenham Hotspur waliopo katika nafasi ya nne na pointi 22 nyuma ya vinara Arsenal.**

"Ni ngumu. Hili ndilo jambo ambalo linanisumbua zaidi kuhusu kutopigania mataji," alisema Casemiro akiiambia ESPN Brazil.

> ●●● Kuwa pointi 20 nyuma ya nafasi ya kwanza, siwezi hata kulala ili kujaribu...

"Kuwa pointi 20 nyuma ya nafasi ya kwanza, wakati mwingine siwezi hata kulala. ili kujaribu kufikiria kufanya kitu tofauti. Ni ukweli. Hakuna maana katika kufikiria kuhusu taji au nafasi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, tunahitaji kufikiria kuhusu michezo ya leo."

"Tunatakiwa kutafakari siku hadi siku, tulipata nafasi ya kupata pointi tisa katika michezo michache iliyopita na tukafunga mbili, tulikasirika, tunapaswa kufikiria mchezo kwa mchezo na kuzingatia mechi ijayo, dhidi ya Bournemouth. "

Kikosi cha Erik ten Hag kimeshuka kwa pointi saba kutoka nafasi za ushindi ndani ya siku nane baada ya kubanwa na Brentford na Chelsea na sare ya mabao 2-2 dhidi ya Liverpool Jumapili.

"Mechi dhidi ya Liverpool ilikuwa ya kasi sana na ilichezwa vema. Mchezo wa kawaida.

"Tulikuwa tunacheza dhidi ya mmoja wa viongozi wa mashindano na ambaye anapitia wakati mzuri. Tulijibu vema," aliongeza Casemiro.

"Timu zote zilikuwa na nafasi. Mchezo ulikuwa mzuri. Nyumbani tuna nguvu, lakini tulicheza dhidi ya timu kubwa. Tunapaswa kufikiria mechi inayofuata."

# RASHFORD KURUDI UWANJANI HARAKA




**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag hataraji Manchester United kuwa bila Marcus Rashford kwa muda mrefu baada ya fowadi huyo kulazimika kutoka nje kwa majeraha katika mchezo wa Jumapili wa sare ya mabao 2-2 na Liverpool.

Rashford alirejea kwenye kikosi cha kwanza baada ya kuachwa katika kichapo dhidi ya Chelsea, lakini alichechemea kipindi cha pili kwenye mchezo dhidi ya Liverpool na nafasi yake kuchukuliwa na Antony.

Majeruhi yameonekana kuwa mengi kwa Ten Hag katika wiki za hivi karibuni, lakini bosi huyo haamini kuwa Rashford anakabiliana na jambo lolote baya.

„Sina uhakika, lakini sidhani kama itakuwa kwa muda mrefu," alisema akiiambia MUTV.

Alisema watajua zaidi hali ya Rashford katika siku zijazo, huku Ten Hag akiwa na matumaini ya kuweza kurudi uwanjani haraka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26.

United watasafiri kumenyana na Bournemouth Aprili 13 kabla ya kuelekeza mawazo yao kwenye nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Coventry siku nane baadaye.

Ten Hag anatarajia kuwakaribisha mabeki wa kati Raphael Varane na Jonny Evans kurejea katika kikosi chake kabla ya mechi ya Kombe la FA, huku mabeki wenzake Victor Lindelof na Lisandro Martinez wakikabiliana na majeraha kwa muda mrefu zaidi nje ya uwanja.

# Rodrygo afunguka kuikatalia Liverpool




**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Rodrygo amekiri kuwa alikataa nafasi ya kujiunga na Liverpool mwaka 2017, miezi 12 kabla ya kuhamia Hispania.

Wakiwa wameonja mafanikio kutokana na usajili wao wa Vinicius Junior mwaka 2017, Madrid walirejea sokoni Brazil ili kumnasa Rodrygo kutoka Santos, na kutumia kitita cha euro milioni 45 ili kumsajili kinda huyo aliyekuwa na umri wa miaka 17.

Tetesi za uwezekano wa kuhamia Ligi Kuu England msimu huu wa majira ya joto zimeibuka hivi karibuni, lakini Rodrygo sasa amefichua jinsi alivyokaribia kuchukua hatua yake ya kwanza Ulaya akiwa na Liverpool baada ya ofa ya dau la euro milioni 3 kukubaliwa.

„Hatukufunga mpango huo kwa sababu sikutaka," alisema Rodrygo. „Nilitaka kubaki Santos ingawa ofa ilikuwa nzuri sana.

"Njia waliyoniahidi pia ingekuwa nzuri sana kwa maisha yangu. Nilikuwa naenda kumalizia masomo yangu Uingereza kujiandaa na soka la Ulaya.

"Siku zote ilikuwa ndoto yangu kucheza Ulaya. Kila kitu kilikuwa kizuri sana, lakini nia yangu ilisikika zaidi. Nilitaka kubaki Santos na kuweka historia katika klabu. Na ndivyo ilivyokuwa: niliweza kutimiza ndoto yangu ya kuichezea Santos, lakini nilikaribia kutua Liverpool."

Rodrygo, ambaye aliruhusiwa kuhamia Ulaya mwaka 2019 mara tu alipofikisha umri wa miaka 18, tangu wakati huo ameweza kucheza mechi zaidi ya 200 akiwa na Madrid, akifunga mabao 52 na asisti 40.

Licha ya kukosa saini ya Mbrazil huyo, Liverpool haikufanya vibaya sana katika dirisha la uhamisho la 2017, ilimnasa Mohamed Salah kutoka AS Roma kwa pauni milioni 34.

Tangu Rodrygo alipohamia Hispania amekabiliana na Liverpool mara tano, akishinda nne - ikiwa ni pamoja na fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu wa 2021/22 - na sare mara moja.

# Havertz aeleza alivyorudisha kiwango

**LONDON,** England

KAI Havertz amefunguka kuhusu mapambano yake ya awali akiwa Arsenal baada ya kufunga bao katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Brighton Jumamosi na kuendeleza kasi yake nzuri.

Wakati mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani Havertz aliposajiliwa kutoka Chelsea msimu wa majira ya joto wa 2023, ilidhaniwa kuwa atachukua nafasi kwenye idara ya kiungo na kweli alianza msimu wa 2023/24, lakini hakuwa kwenye kiwango bora.

Hata hivyo, tangu wakati huo amecheza kwa kiasi kikubwa kama mshambuliaji na kuwa mchezaji mahiri wa kufunga mabao, akitikisa nyavu mara tisa katika mechi 30 za Ligi Kuu msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliiambia Sky Sport kwamba, sasa anajisikia ‚furaha sana' ndani ya kikosi cha ‚Washika-bunduki' hao licha ya kuhitaji muda kutulia.

Alisema: „Kwangu, nilipohamia Chelsea mwaka 2020 ilikuwa kawaida kwamba ulihitaji muda kidogo kufika na kujuana na kila mtu ipasavyo na kuwa na uhusiano mzuri uwanjani. Na ilikuwa wazi mimi kwamba itachukua wiki chache.

„Mimi ni mtu ambaye sijitokezi kwa urahisi katika mazingira mapya, lakini kwangu mimi huchukua wiki chache au miezi michache.

"Najisikia furaha sana. Naipenda klabu. Nawapenda wachezaji, wafanyakazi na ninawapenda mashabiki kwa hiyo kwangu lilikuwa jambo sahihi kabisa kufanya na nina furaha tu.

„Kuwa hapa na kupigania mataji mwaka huu. Bado tuna mataji mawili ambayo tunaweza kushinda na sasa wiki muhimu za msimu zinaanza na mimi binafsi na bila shaka timu nzima itafanya kila kitu kushinda mataji."



# HABARI MICHEZO

## Maxime aianzia kazi Simba SC

Na Saada Akida

BAADA ya kujihakikishia kucheza robo fainali ya Kombe la CRBD Bank Federation, Kocha Mkuu wa Singida Black Stars ( zamani Ihefu FC), Mecky Maxime, sasa ameanza kuipigia hesabu Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Singida Black Stars watakuwa nyumbani kuwakaribisha Simba katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu utakaochezwa Aprili 13, mwaka huu, katika dimba la Liti liliopo mjini Singida.

Akizungumza na Nipashe jana, Mecky alisema baada ya kufanikiwa kufuzu robo fainali wamerejea uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yao kujiandaa katika mchezo ujao dhidi ya Simba.

Alisema ligi inaelekea ukingoni na michezo ya mwisho inakuwa ya ushindani mkubwa kwa kila timu kuhitaji kupambana kusaka pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuendelea kusalia kwenye Ligi Kuu.

"Tunatambua tuna mechi ngumu mbele yetu, tunahitaji kufanya maandalizi mazuri, kusahihisha makosa yetu yaliyojitokeza kwenye michezo iliyopota, kujiandaa na mechi zijazo ikiwamo dhidi ya Simba," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa mipango yao ni kuhakikisha wanafanikiwa kukusanya pointi katika kila mchezo kwa kujiweka katika mazingira mazuri ya kumaliza ligi katika nafasi tano za juu.

Singida Black Stars wako nafasi ya 11 wakiwa na pointi 23, wamecheza michezo 21, wameshinda sita, sare tano na kupoteza mechi 10.



# CHE MALONE BADO YUPO SANA SIMBA

Na Adam Fungamwango

BAADA ya tetesi kuwa beki wa kati wa Simba, Che Fondoh Malone, kuwa anataka kuondoka kwenye klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu, wakala wa mchezaji huyo, Amadou Fontem Tigana, amesema mchezaji huyo atasalia kwenye kikosi hicho kipindi chake chote cha mkataba, labda klabu yenyewe imuuze.

Akizungumza kutoka nchini Cameroon, kutokana na madai hayo, alisema baadhi ya wanahabari walimnukuu vibaya, badala yake alisema atacheza kwa juhudi kubwa ili klabu kubwa zimnunue.

**"Hajasema kuwa haipendi Simba na wala hataki kuondoka Simba, bali watu wamemtafsiri vibaya, alichosema ni kwamba atacheza kwa juhudi ili klabu kubwa zimnunue," alifafanua wakala huyo.**

Ufafanuzi huo unakuja siku moja tu baada ya baadhi ya vyombo vya habari kudai kuwa beki huyo aliyejiunga na klabu hiyo mwanzoni mwa msimu huu akitokea Coton Sports ya Cameroon, kuripoti kuwa ameandika barua ya kuomba kuondoka klabuni hapo mara baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu msimu huu.

Msimu utakapomalizika, mchezaji huyo aliyesaini mkataba wa miaka miwili, atabakisha msimu mmoja, hivyo klabu yoyote inayomhitaji itabidi iongee na Simba.

Huyo ni mchezaji wa pili wa Simba kuhusishwa kuondoka mwishoni mwa msimu, baada ya beki mwingine wa kati, Henock Inonga, kudaiwa kutakiwa na Klabu ya FAR Rabati ya Morocco inayonolewa na Kocha wa zamani wa Yanga, Nasreddine Nabi.

## ARSENAL DAY...



Wazazi waishio eneo la Masaki jijini Dar es Salaam, wakishindana na watoto wao kuvuta kamba wakati wa Tamasha la Siku ya kuzaliwa mashabiki wa timu Arsenal akiwamo Kasinge Johnson a.k.a Saka, watoto hao waliwashinda wazazi katika mchezo huo wa kuvuta kamba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Simba yafia tena kwa Mashujaa FC*

INATOKA UK. 24

mechi ya mkondo wa kwanza ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Lusajo aliunganishwa mpira wa kona iliyopigwa na Mpoki Mwakinyuke ambayo ilipita kwenye msitari wa wachezaji wa Simba ambao wengine hawakuruka na wengine walifanya hivyo kivivu na kwenda kwenye nguzo ya pili kumkuta mfungaji aliyeukwamisha wavuni kwa kichwa kirahisi.

Kuingia kwa bao hilo kulionekana kama kuwashangaza, kuwaduwaza na kuwahuzunisha wachezaji wa timu hiyo kwani baada ya hapo walionekana kupoteana na kuwapa nafasi wenyeji wao kuwashambulia mfululizo.

Kama Mashujaa FC wangekaa vema dakika kadhaa baada ya ya kupata bao wangeweza kufunga mengine mawili, kwani Omari Omari aliwakosa Simba dakika ya nane, na dakika ya 11, Adam Adam alibaki peke yake na kipa Ali Salim, lakini mpira uliishia mikononi mwa mlinda mlango huyo.

Hatimaye Simba ilifanya shambulizi la nguvu langoni kwa Mashujaa, dakika ya 21, Kibu Denis aliachia shuti kali lakini liliwababatiza mabeki na kwenda pembeni ya uwanjani ambako aliufuata na kuutumbuliza ndani mpira ambao haukutendewa haki na Saido Ntibazonkiza.

Kama angekuwa makini, Fabrice Ngoma, angeisawazishia Simba bao dakika ya 26, alipounganisha mpira wa faulo iliyopigwa na Clatous Chama, lakini mpira wake ulipaa juu kiasi cha hatua tatu kutoka langoni.

Golikipa wa Mashujaa, Erick Johora, alifanya kazi ya ziada dakika ya 39, aliporuka juu na kuupangua mpira uliokuwa unaelekea wavuni, ukipigwa na Babakar Sarr kwa kichwa, aliyeunganisha mpira wa kona kutoka kwa Saido.

Dakicha chache kabla ya mechi kwenda mapumziko, kiungo mkabaji wa Mashujaa, Said Makapu, alionyeshwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya, Saido, ambapo mwanzo alimchezea kama hivyo, Clatous Chama na kupata kadi ya njano.

Mabadiliko ya kumtoa Pa Omar Jobe na kumuingiza, Freddy Michael na wengine kipindi cha pili yalisaidia Simba kwa Freddy kuisawazisha bao dakika ya 51, huku akikosa mawili ya wazi dakika za mwanzo tu alizoingia na ya 71, pamoja na Kibu, ambaye alipiga shuti kali dakika ya 73, lakini Johora alikaa imara, licha ya timu yake kuwa pungufu waliweza kuwabana Simba na kwenda nao hatua ya matuta baada ya sare hiyo ya bao 1-1.

## Yanga: Ni ushindi tu Kombe la FA leo

INATOKA UK. 24

"Kuna tofauti, tunawaheshimu wapinzani wetu na tutacheza kwa tahadhari kubwa kwa namna yoyote mchezo utakuwa mgumu na ushindani mkubwa," alisema Gamondi.


Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Francis Baraza, alisema wachezaji wake wapo tayari kwa mchezo huo na anatumai utakuwa mgumu kwa sababu hawako tayari kupoteza mara mbili mbele ya wapinzani wao hao.

Alisema ameiona Yanga ilivyocheza katika mechi zake za kimataifa, lakini hao ni mabingwa watetezi wa Kombe la Shirikisho, hivyo wanapaswa kucheza kwa tahadhari kubwa ili kupata ushindi.

"Tunawaheshimu Yanga, ni timu kubwa imetoka kutolewa kwenye michuano mikubwa, wataingia katika mchezo huu kivingine, lakini hatutakuwa tayari kupoteza mara mbili mbele ya wapinzani wetu hao," alisema Baraza.

# Michezo

Jumatano Aprili 10, 2024
Nipashe



Casemiro: Man Utd inanikosesha usingizi UK. 21




# Simba yafia tena kwa Mashujaa FC

## ●●● Yatolewa Kombe la FA, sasa matumaini pekee Ligi Kuu Bara...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena Simba imetolewa na Mashujaa FC kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu CRDB Confederation Cup kwa mikwaju ya penalti 6-5, katika mechi ya hatua ya 16-bora iliyochezwa jana, Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma.

Mashabiki wa Simba jana walikumbushwa uchungu walioupata, Desemba 26, 2018 kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, ilipotolewa na Mashujaa kwa jumla ya mabao 3-2, katika Raundi ya Tatu ya michuano hiyo, wakati huo ikiwa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara kwa mabao yaliyofungwa na Shabani Hamis na Jeremiah Josephat aliyefunga mawili, ya Simba yakifungwa na Paul Bukaba na Clatous Chama ambaye alikuwapo jana katika mechi nyingine ya kombe hilo.

**Timu hizo zililazimika kupigiana penalti baada ya kutoka sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90 za mchezo.**

Kipa Erick Johora, aliibuka kuwa shujaa katika mchezo wa jana akipangua penalti mbili za Simba zilizopigwa na wachezaji wa kigeni, Mcameroon Willy Onana na raia wa Mali, Sadio Kanoute, huku Mashujaa ikikosa penalti moja tu iliyopigwa na Zuberi dabi ambayo ilipaa juu ya lango.

Penalti za washindi ziliwekwa kimiani na Samson Madeleke, Michael Masinda, Mohamed Stambuli, Adam Adam, Mpoki Mwakinyuke na Bakari Mtui, huku za Simba zikitumbukizwa kimyani na Mohamed Hussein ‚Tshabalala‘, Israel Mwenda, Freddy Michael, Mzamiru Yassin na Ladack Chasambi.

‚Wekundu wa Msimbazi‘ wametolewa kwenye michuano hiyo, siku nne tu baada ya kuondoshwa pia kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly, hivyo kupoteza taji la pili msimu huu, ambapo sasa mategemeo yote ni ubingwa wa Tanzania Bara, ikiwa na taji moja tu mpaka sasa ambalo ni Ngao ya Jamii, ililolipata, Agosti 13, mwaka jana kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, ilipoifunga Yanga kwa mikwaju ya penalti 3-1 baada ya kutoka suluhu ndani ya dakika 90.

Utamaduni wa Simba kuruhusu mabao ya mapema, uliendelea jana dakika ya tano tu ilipofungwa bao na straika mzoefu, Realiants Lusajo, muda ambao pia iliadhibiwa na Al Ahly ya Misri kwenye

INAENDELEA UK. 23

# Yanga: Ni ushindi tu FA leo

**Na Saada Akida**

WAKATI mabingwa watetezi wa Kombe la Shirikisho la Soka nchini (CRBD Bank Federation Cup), Yanga, leo wakitarajiwa kushuka dimbani katika mchezo wa hatua ya 16-bora dhidi ya Dodoma Jiji FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, amesema hakuna namna ya kusonga mbele zaidi ya ushindi.

Timu hizo ambazo zitakutana katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, zimeshakutana mara tano kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, na hii ni mara ya kwanza kwao kukutana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho.

Katika mara tano zilizokutana, Yanga imeshinda mechi zote na mara ya mwisho zilipokutana mabingwa hao watetezi wa CRBD Bank Federation Cup, walipata wakati mgumu na kuondoka na ushindi wa bao 1-0, mchezo uliopigwa Februari 5, mwaka huu.

Hata hivyo, katika mchezo wa leo Yanga inahitaji ushindi ili kuendelea kujihakikishia kutetea taji lao huku Dodoma jiji FC nayo ikihitaji kushinda kwa ajili ya kwenda kucheza robo fainali ya michuano kwa mara ya kwanza katika historia ya timu hiyo.

Itakayoshinda katika mchezo wa leo itakwenda kuungana na timu sita ambazo zimekwishatinga robo fainali ambazo ni Azam FC, Singida Black Stars zamani Ihefu FC, Coastal Union, Namungo FC, Geita Gold na Tabora United.

Kuelekea mchezo huo Kocha wa Yanga, Gamondi amesema wanatambua ugumu wa mashindano hayo hasa hatua za mtoano kwa kuwa lazima kushinda na na hicho ndicho wanachokitaka leo.

Alisema kwenye mashindano ya mtoano ushindi ndio unaohitajika ili kusonga mbele hatua inayofuata, hivyo hakuna namna lazima kupata ushindi.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042